# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI MHESHIMIWA DKT. SHUKURU JUMANNE KAWAMBWA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/16

**JUNI, 2015**

# I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii iliyochambua na kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2015/16.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutimiza majukumu yangu kama Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki aliyeteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na hivyo kuwa msaidizi wangu mkuu katika kusimamia elimu nchini. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja, (Mb.) na Mheshimiwa

Innocent Sebba, (Mb.) walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kupata fursa ya kuchangia maendeleo ya Taifa kwa kuwakilisha Wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Katibu Mkuu, Profesa Sifuni Ernest Mchome; Naibu Katibu Mkuu, Bibi Consolata Philipo Mgimba; Kamishna wa Elimu, Profesa Eustella Peter Bhalalusesa; Wakurugenzi; Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi za elimu zilizo chini ya Wizara yangu kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara na kuandaa bajeti hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wahadhiri, Wakufunzi, Walimu na Watumishi wote kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Napenda pia kuwashukuru, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zisizo za Serikali, Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Wanataaluma, Wanafunzi na Wazazi/Walezi kwa ushirikiano wao katika kuiendeleza Sekta ya Elimu nchini.

4. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kutoa salamu za pole kwako na kwa Bunge lako Tukufu kwa kifo cha Mbunge mwenzetu mpendwa, Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba, aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi. Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote waliofiwa na ndugu na wapendwa wao kutokana na maradhi, ajali, majanga na matukio mbalimbali yaliyotokea katika nchi yetu. Namwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi pamoja na kuwapa faraja wote walioondokewa na wapendwa wao.

# II. MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

5. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Hati Idhini iliyounda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 17 Desemba, 2010 na urekebishaji wa muundo wa wizara uliofanyika mwaka 2015 na kuidhinishwa na Mhe. Rais, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ina majukumu yafuatayo:

    a) utungaji wa Sera za Elimu zinazohusu Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Elimu ya Juu na Elimu ya Watu Wazima;

    b) utekelezaji wa Sera za Elimu katika maeneo ambayo ni ya Wizara;

    c) mafunzo ya Ualimu;

    d) usajili wa Shule;

    e) usimamizi wa Ubora wa Elimu ikiwemo wa elimumsingi;

    f) uchapaji wa machapisho ya Elimu;

    g) usimamizi wa huduma za Maktaba;

h) uratibu wa shughuli zinazotekelezwa na Kamisheni ya Taifa ya UNESCO;

i) uratibu wa shughuli za Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara;

j) usimamizi wa utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya Wizara; na

k) uendelezaji wa rasilimaliwatu na uongezaji tija ya watumishi walio chini ya Wizara.

# III. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2014/15

6. **Mheshimiwa Spika**, naomba nianze kwa kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/15 kuanzia tarehe 1 Julai, 2014 hadi tarehe 30 Aprili, 2015.

## Ukusanyaji wa Maduhuli Mwaka 2014/15

7. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Wizara yangu ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi **213,447,418,474.00** ambapo shilingi **9,108,383,900.00** zilipangwa kukusanywa na Idara na shilingi **204,339,034,574.00** zilipangwa kukusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi tarehe 30 April, 2015 kiasi cha maduhuli yaliyokusanywa ni Shilingi **162,811,384,265.97** sawa na asilimia **76.3** ya makadirio. Kati ya makusanyo hayo, Shilingi **5,136,353,002.60** zilikusanywa na Idara na shilingi **157,675,031,263.37** zilikusanywa na Taasisi. Kiasi kikubwa cha maduhuli kilitokana na malipo ya ada na huduma mbalimbali za kielimu zilizotolewa na Idara na Taasisi za Elimu na Mafunzo.

## Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2014/15

8. **Mheshimiwa Spika**, mwaka wa fedha 2014/15, bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa na bunge lako tukufu, ilikuwa shilingi **344,207,056,000.00**. Kutokana na marekebisho ya bajeti kwa wizara zote (Budget Cut-off), kiasi cha shilingi **2,423,036,000.00** kilipunguzwa kutoka kwenye bajeti ya Wizara. Aidha, katika robo ya pili, bajeti ya Wizara iliongezwa kwa shilingi **4,490,000,000.00** kwa ajili ya kulipia deni la 'Inter University Council for East Africa' na kufikia shilingi **346,274,020,000.00**. Kati ya fedha hizo, mishahara ilikuwa shilingi **268,756,248,000.00** ambapo Mishahara ya Idara ilikuwa shilingi **52,976,832,000.00** na ya Taasisi ilikuwa shilingi **215,779,416,000.00**. Matumizi Mengineyo ilikuwa shilingi **77,517,772,000.00** ambapo shilingi **53,586,982,000.00** zilikuwa kwa ajili ya Idara na shilingi **23,930,790,000.00** kwa ajili ya Taasisi.

9. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2015, kiasi cha shilingi **286,043,459,577.02** sawa na asilimia **83.1** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida kimepokelewa na kutumiwa na Wizara

yangu. Kati ya fedha hizo, shilingi **238,592,738,417.67** ni za mishahara ambapo shilingi **46,806,528,214.67** ni za Idara na shilingi **191,786,210,203.00** ni za Taasisi. Matumizi Mengineyo ni shilingi **47,450,721,159.35** ambapo shilingi **22,637,145,706.35** zimetumiwa na Idara na shilingi **24,813,575,453.00** zimetumiwa na Taasisi.

10. **Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha za Matumizi Mengineyo zilizopokelewa, shilingi **17,556,516,175.35** zilitumika kulipa madeni ya baadhi ya Taasisi na ya Wizara ambayo yalikuwa tayari yamehakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali ambapo shilingi **8,956,743,006.65** ni madeni ya Taasisi na shillingi **8,599,773,168** madeni ya wizara.

## Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2014/15

11. **Mheshimiwa Spika**, mwaka wa fedha 2014/15, jumla ya shilingi **454,813,333,000.00** ziliidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa ajili ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Wizara yangu. Hata hivyo kiasi cha shilingi

**1,200,000,000.00** kilipunguzwa na kufikia shilingi **453,613,333,000.00**, ambapo fedha za ndani zilikuwa shilingi **383,734,000,000.00** na fedha za nje shilingi **69,879,333,000.00.** Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2015, jumla ya shilingi **335,003,135,231.66** sawa na asilimia **73.9** zilikuwa zimepokelewa ambapo shilingi **305,822,570,000.00** ni fedha za ndani na shilingi **29,180,565,281.66** ni fedha za nje.

## Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2014/15

12. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu ni moja ya wadau wakubwa wa sekta ya elimu ambayo ilijiwekea vipaumbele vikuu viwili katika mwaka wa fedha 2014/15. Vipaumbele hivyo ni:

    a) kuinua ubora wa elimu na kujenga stadi stahiki katika ngazi zote za elimu na mafunzo; na

    b) kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu kwa usawa katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

13. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa vipaumbele vya sekta, Wizara yangu

ilifanya kazi kwa kushirikiana na wadau wengine hususan Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM - TAMISEMI) ambayo ndiyo yenye wajibu wa kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhusu elimu ya msingi na sekondari. Aidha, Wizara na Taasisi zenye shule na vyuo pamoja na Taasisi zisizo za serikali ambazo zinamiliki na kuendesha shule na vyuo mbalimbali nchini pia zilishiriki kikamilifu katika kutimiza azma ya Serikali ya kutoa elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali, ikiwemo Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi.

14. **Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii sasa kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu kulingana na Hati Idhini ya Wizara yangu katika kutekeleza vipaumbele vya sekta ya elimu.

## ***Utungaji wa Sera za Elimu***

15. **Mheshimiwa Spika,** moja ya majukumu ya Wizara yangu ni kubuni na kutunga sera mbalimbali kuhusu elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Juu. Lengo la sera hizi ni kutoa

mwelekeo katika kutekeleza majukumu ya uendeshaji wa elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali. Katika eneo hili mwaka wa fedha 2014/15, Wizara yangu imefanya yafuatayo:

a) ilikamilisha Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 13 Februari 2015 na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Mkakati wa Utekelezaji wa sera unahakikiwa na wadau ili utekelezaji wake uanze mwaka wa fedha 2015/2016;

b) rasimu ya andiko la uanzishwaji wa Bodi ya Kitaalam ya Walimu imekamilika. Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuanzisha Bodi ya Kitaalam ya Walimu umeandaliwa na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Kitaalam ya Makatibu Wakuu wa Wizara (IMTC);

c) mtaala wa Darasa la I na II umeandaliwa kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mtaala wa mwaka 2005. Aidha, viunzi na miongozo mbalimbali kuhusu ufundishaji mahiri wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) vimeandaliwa;

d) Waraka wa Elimu Na. 4 wa mwaka 2014 unaoipa Taasisi ya Elimu Tanzania jukumu la kuandika vitabu vya kiada na kuratibu utayarishaji na utoaji wa Ithibati kwa vitabu vya ziada na vifaa vingine vya kujifunzia kwa ngazi ya elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu umetolewa. Aidha, Mwongozo wa hatua zinazotakiwa kufuatwa katika utoaji ithibati kwa vitabu na vifaa vya kielimu kwa ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu umetolewa pia;

e) ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sera za elimu na mafunzo umeimarishwa kwa kuandaa na kutoa nyaraka zifuatazo:

    i. Waraka wa Elimu Na. 3 wa mwaka 2014 kuhusu Vibao vya Maelekezo Mahali Shule ilipo;
    ii. Waraka wa Elimu Na. 1 wa mwaka 2015 kuhusu Kalenda ya Mihula kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari;
    iii. Waraka wa Elimu Na. 3 wa mwaka 2015 kuhusu Vigezo vya Udahili wa Wanafunzi wa Kidato cha Tano;

f) mkakati wa kuhuisha na kuoanisha programu za Elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira umeendelea kutekelezwa kwa kufanya yafuatayo:

   i. chini ya uratibu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania (Bara na Zanzibar) ilishiriki kuandaa na kukamilisha miundo ya mitaala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (East Africa Curriculum Structures and Frameworks) kwa elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari na Ualimu wa Elimu ya Msingi na Sekondari pamoja na muundo wa viwango vya Elimu ya Juu (East Africa Higher Education Qualification Framework). Miundo hii imepitishwa na kikao cha **12** cha Baraza la Mawaziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Utamaduni na Michezo lililokutana Machi, 2015;

   ii. Tanzania ilishiriki katika kupitia Itifaki na miswada ya Inter-University of East Africa (IUCEA) ambayo imeidhinishwa na Baraza la Mawaziri lililokutana Machi, 2015;

iii. vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika fani za Biashara na TEHAMA vilivyoandaliwa chini ya uratibu wa IUCEA vimekamilika. Vyuo na Taasisi za Ithibati (NACTE na TCU) vimeanza kutumia vigezo hivyo katika kupitia mitaala ya Biashara na TEHAMA;

iv. Tanzania pia ilishiriki kuandaa na kukamilisha sheria na kanuni za uendeshaji mitihani kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

v. Mitaala **10** ya kitaifa (**7** ngazi ya Astashahada na Stashahada, **3** Stashahada ya Juu) na mitaala **60** (**41** ngazi ya Astashahada na Stashahada, **16** ngazi ya Shahada na **3** ngazi ya Shahada ya Uzamili) ya Vyuo vya elimu ya ufundi inayozingatia umahiri na mahitaji halisi ya soko la ajira na maendeleo ya taifa imetayarishwa na kuidhinishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

## Usajili wa Shule

16. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mfumo wa usajili wa shule, Kitengo cha Usajili wa Shule kimepandishwa hadhi kuwa Idara ya Ithibati ya shule yenye vitengo vitatu ambavyo ni Ithibati ya Shule za Serikali, Ithibati ya Shule zisizo za Serikali na Uwekaji Viwango vya Miundombinu ya shule chini ya Ofisi ya Maendeleo ya Elimu msingi. Aidha, taratibu za kuhuisha mfumo wa usajili na utunzaji kumbukumbu za shule na walimu kwa njia ya kielektroniki unaandaliwa.

17. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kusajili shule kwa lengo la kuzipatia ithibati na idhini ya kufundisha masomo husika. Mwaka wa fedha 2014/15, Shule za Awali na Msingi **60** zilisajiliwa. Kati ya hizo, shule **57** ni za Binafsi na 3 za Serikali ambapo shule binafsi za Awali pekee ni mbili (2) na Shule za Msingi pekee mbili (2). Aidha, Shule za Sekondari **45** zilisajiliwa kati ya hizo shule **12** ni za Serikali na **33** za Binafsi. Shule **32** ni za kidato cha I – IV na **13** za kidato cha V-VI. Shule zote za Kidato cha V - VI zimejumuisha michepuo ya masomo ya Sayansi.

## ***Uthibiti Ubora wa Elimu Msingi***

18. **Mheshimiwa Spika,** Uthibiti Ubora elimu msingi ni jambo muhimu sana katika kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa katika ngazi hiyo. Hadi kufikia Aprili, 2015, yafuatayo yametekelezwa:
    a) Asasi **11,531** kati ya **17,021** zilizolengwa sawa na asilimia **67.7** zilifanyiwa tathmini ya kuthibiti ubora. Asasi hizo zilijumuisha shule za Awali na Msingi **8,197**, Sekondari **3,222** na Vyuo vya Ualimu **112**; na
    b) Mfumo wa Uthibiti Ubora wa kielektroniki (Inspectorate Management Information System – IMIS) unatengenezwa kwa kufanya majaribio katika wilaya saba (7) za Magu, Mtwara (V), Bagamoyo, Makete, Temeke, Siha na Hai. Mfumo huu utakapokamilika utasimikwa katika wilaya zote ili kusaidia kusambaza taarifa za ukaguzi kwa wadau wengi na kupata mrejesho kwa wakati.
19. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha Uthibiti Ubora wa Elimu msingi, Ofisi za Uthibiti Ubora zimefunguliwa katika Halmashauri 8 za Wilaya mpya za Kaliua,

Njombe (M), Wanging'ombe, Makambako, Nyang'wale, Busega, Geita (M) na Nyasa. Ofisi katika wilaya nyingine zitaendelea kufunguliwa kwa awamu. Aidha, Walimu **217** wameteuliwa kuwa Wathibiti Ubora wa Elimu msingi na kupangwa katika ofisi za Ukaguzi wa shule za Kanda na Wilaya, Magari mawili (2) yamenunuliwa na 45 yapo katika hatua za mwisho za ununuzi kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi katika ofisi za Kanda na Wilaya. Vilevile, nafasi za Uthibiti Ubora wa Elimu msingi wa Wilaya na Kanda zimeingizwa katika muundo wa mshahara wa viongozi wa Serikali (LSS – E) ili kuimarisha usimamizi katika utendaji kazi. Utekelezaji wake utaanza tarehe 01 Julai 2015. Aidha, katika kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini, Idara ya Ukaguzi wa Shule imepandishwa hadhi kuwa idara ya Uthibiti Ubora wa Elimu msingi ambapo itakuwa na watendaji hadi ngazi ya kata.

## ***Mafunzo ya Ualimu***

20. **Mheshimiwa Spika,** mafunzo ya ualimu yaliendelea kutolewa katika vyuo vya Serikali na vya binafsi na kuwezesha upatikanaji wa walimu wenye sifa na weledi na kukabiliana na upungufu wa

walimu hususan wa masomo ya Sayansi na Hisabati. Katika mwaka 2014/15 yafuatayo yametekelezwa:

a) programu ya mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati ya Miaka 3 kwa wahitimu wa kidato cha IV wenye ufaulu wa daraja la 1-3 imeanzishwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Wanachuo **2,142** wamedahiliwa katika mwaka wa masomo 2014/15 (**1,964** Stashahada ya Elimu ya Sekondari na wanachuo **178** Stashahada ya Sayansi Shule za msingi);

b) Stashahada ya Juu ya Masomo ya Sayansi na Hisabati kwa ajili ya shule za Sekondari imeanzishwa katika vyuo vya ualimu vya Korogwe, Monduli na Kleruu ambapo jumla ya wanachuo **365** wamedahiliwa;

c) wawezeshaji wa kitaifa **24** wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wakufunzi wa walimu wa darasa la I & II kumudu stadi za KKK. Aidha, Wakufunzi **480** wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wa darasa la I & II kufundisha stadi za KKK;

d) vyuo vya ualimu vimepandishwa hadhi ambapo sasa vitapewa ithibati ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi badala ya kusajiliwa na ofisi ya Kamishna wa Elimu. Kutokana na utaratibu huo, hadi sasa vyuo **29** vya Serikali vya Ualimu vimepata usajili kamili na chuo **1** usajili wa muda na kupewa miongozo ya kupata ithibati. Vyuo **4** vya Mpuguso, Kitangali, Ndala na Shinyanga bado havijapatiwa usajili kutokana na kutokidhi vigezo. Wizara inaendelea na taratibu za kukamilisha vigezo husika ili vyuo hivyo viweze kusajiliwa na kupewa miongozo ya kupata ithibati;

e) kanuni (Establishment Orders) zimeandaliwa chini ya sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kwa ajili ya kuviwezesha vyuo sita vya Ualimu vya Nyanza (Butimba), Lake Tanganyika (Kasulu), Klerruu, Morogoro, Mtwara na Patandi kujitegemea kiutendaji. Kanuni hizo zimewasilishwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya utaratibu wa kuzitangaza kwenye gazeti la serikali kwa mujibu wa sheria;

f) mfumo wa kielektroniki wa kudahili (online application system) wanafunzi wa kujiunga na mafunzo ya ualimu ngazi ya stashahada umekamilika na kutumika kwa majaribio kwa programu ya Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mfumo huu utatumika kudahili wanafunzi wa ualimu mwaka 2015/16 kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kudahili;

g) Serikali imepata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na Serikali ya Canada ambazo zitawezesha kuhuisha mtaala wa Stashahada ya Ualimu na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika vyuo vya ualimu pamoja na kukarabati vyuo vya ualimu vya Shinyanga, Mpuguso, Ndala, Kitangali, Tabora, Mpwapwa, Butimba, Dakawa, Marangu na Klerruu; na

h) Serikali imepata msaada kutoka Serikali ya China kupitia UNESCO kwa ajili ya uimarishaji wa tasnia ya ualimu katika matumizi ya TEHAMA ambapo vyuo viwili vya ualimu vya Tabora na Monduli vitatumika kwa ajili hii.

## ***Uratibu wa Taasisi na Wakala***

21. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu ina jumla ya Taasisi na Wakala **89** za elimu na mafunzo. Kati ya hizo: **3** ni za ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu ya ufundi stadi, elimu ya ufundi na elimu ya juu, **2** ni za mitaala na mitihani, **2** za mikopo na ruzuku mbalimbali, **1** ni bodi ya huduma za maktaba, **1** ni Tume ya Taifa ya UNESCO na kituo **1** cha Hazina Data kilichopo Kituo cha Maendeleo Dakawa. Aidha, zipo Taasisi za mafunzo **79** zikiwemo **28** zinazoendeshwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Mafunzo ya ufundi Stadi. Taasisi na Wakala hizi zilitekeleza majukumu yake kulingana na sera za elimu na mafunzo, miongozo inayotolewa mara kwa mara na serikali na taratibu za taasisi hizo. Aidha, zilichangia kuleta ubora wa elimu na kutoa fursa sawa katika utoaji elimu na mafunzo. Taasisi hizo zilitekeleza yafuatayo:

## ***Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)***

22. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi hii ina jukumu la kutoa mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, kufanya utafiti na kutoa ushauri elekezi katika

eneo hili. Katika mwaka 2014/15, *Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima*, ilitekeleza yafuatayo:

a) ilisajili wanafunzi **100** ngazi ya Astashahada, **624** ngazi ya Stashahada na **241** ngazi ya Shahada. Kati yao **87** ni wa shahada ya programu mpya ya Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii;

b) iliandaa na kusambaza nakala **750** za miongozo ya kuanzisha na kuendesha vituo vya masomo nje ya mfumo rasmi katika mikoa yote;

c) iliendesha mafunzo elekezi kwa wakufunzi wakazi wa mikoa **21** wa Elimu ya Watu Wazima na waendeshaji wa vituo **300** ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa vituo;

d) ilikamilisha mihtasari ya masomo ya Fizikia na Kemia hatua ya 2 na kuanza maandalizi ya mihtasari ya masomo ya Biashara;

e) iliandaa moduli **80** (**31** za ufundi wa awali, **10** za stadi nyenzo na **39** za taaluma) za Mpango wa Elimu Changamani baada ya Msingi (MECHAM) kwa kushirikiana na UNICEF kwa ajili ya vituo vipya vya wilaya za Mbeya Vijijini, Mbarali, Iringa Vijijini,

Mufindi, Njombe, Makete na vituo vya awali vya Wilaya za Temeke, Bagamoyo, Mtwara vijijini, Makete, Magu, Siha na Hai. Aidha, Wanafunzi **162** wa mpango changamani katika vituo vya Angaza Siha, Igogo na Buhongwa Mwanza wamefanya mitihani ya ufundi wa awali katika fani za mapishi, Ufundi Magari na Uashi, Ushonaji na Menejimenti ya Hoteli kwa mara ya kwanza; na

f) iliratibu uendeshaji wa masomo katika vituo **10** vya Mpango wa Elimu Mbadala kwa wasichana **147** walioacha shule kwa sababu za uja uzito katika Halmashauri za Wilaya za Shinyanga Vijijini na Msalala. Aidha, mitihani ya masomo ya utangulizi na stadi nyenzo imefanyika katika vituo hivyo.

***Taasisi ya Elimu Tanzania***

23. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi hii ina jukumu la kubuni na kuandaa mitaala na mihtasari ya elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu na Elimu Maalumu. Katika mwaka 2014/15, *Taasisi ya Elimu Tanzania* ilitekeleza yafuatayo:

a) iliandaa mtaala wa Darasa la I & II wenye kuzingatia ukuzaji wa Stadi

za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu pamoja na mihtasari na miongozo kwa ajili ya masomo ya Darasa la & II. Aidha, wakufunzi **480** wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wa Darasa la I & II kufundisha stadi za KKK; na

b) iliandika vitabu **6** vya kiada na elekezi vya Darasa la I. Vitabu hivyo ni: Najifunza Kusoma Kitabu cha I, Najifunza Kusoma Kitabu cha II, Najifunza Kuandika, Najifunza Kuhesabu, Najifunza Afya na Mazingira, Najifunza Michezo na Sanaa.

## ***Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania***

24. **Mheshimiwa Spika,** Bodi hii ina jukumu la kuanzisha, kusimamia, kuongoza, kuimarisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma, kuanzia ngazi za Vijiji, Wilaya hadi Mikoa, kutoa mafunzo na kuendesha mitihani ya Taaluma ya Ukutubi. Katika mwaka 2014/15, *Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania*, ilitekeleza yafuatayo:

a) ilitoa mafunzo kwa wanafunzi **1,071** (Cheti **457**; kati yao wasichana **322** na wavulana **135**; Stashahada **414**; kati yao wasichana **279** na wavulana **135** na Kozi ya miezi mitatu “Elementary Library

Course" **200**; kati yao wasichana **161** na wavulana **39**);

b) ilitoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba katika shule **107**, zikiwemo **46** za msingi na **61** za sekondari, vyuo **7** vikiwemo: Chuo cha Maendeleo ya Jamii - Nzega, Chuo cha Uuguzi Kisare -Manyara, Chuo cha Madini - Mwanza, Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia – Jomo Kenyatta – Tawi la Arusha, Chuo cha Utalii na Uandishi wa Habari - Mbeya, Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Masasi, Chuo cha Mafunzo ya Jeshi Monduli - Arusha na Halmashauri za Wilaya **5** ambazo ni Tunduma; Nachingwea; Temeke; Ileje na Bukombe;

c) imeimarisha huduma za maktaba kwa kuongeza vitabu **205,974** na hivyo kufanya idadi ya vitabu vyote katika Maktaba nchini kufikia **1,474,584**;

d) ilishirikiana na Halmashauri za wilaya za Ruangwa, Chunya, Masasi, Mbulu na Ngara katika kuimarisha maktaba mpya zilizoanzishwa katika Halmashauri hizo. Ilisambaza jumla ya vitabu **22,850** katika Halmashauri za wilaya za Ruangwa,

Chunya, Masasi, Mbulu na Ngara; vikiwemo **12,283** vya masomo shule ya msingi (Hisabati **2,830**; Kiingereza **3,900**; Jiografia **2,470** na Sayansi **3,083** na vitabu **10,567** vya masomo shule za sekondari (Fizikia **2,438**; Kemia; **4,459**; Hisabati **3,100** na Kiingereza **570)**; na

e) ilishirikiana na Shirika la Msaada wa vitabu la Uingereza (BAI), katika kukarabati Vitengo vya Watoto pamoja na kununua samani, vitabu na vifaa vya kielektroniki katika maktaba za mikoa ya Mtwara, Kagera, Tanga, Kilimanjaro na Kibaha pamoja na kuwapa mafunzo maalum watumishi **10** juu ya kuendesha Vitengo vya Watoto katika maktaba za Umma.

## ***Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu***

25. **Mheshimiwa Spika,** Wakala una majukumu makuu ya kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu; kufanya utafiti, kuandaa na kusambaza makala na vitabu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu. Katika mwaka 2014/15, *Wakala*

*wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu*, ulitekeleza yafuatayo:

a) ulitoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa wanafunzi **811** katika vituo vya Bagamoyo na Mwanza yenye lengo la kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shule;

b) ulitoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa wanafunzi **123** katika vituo vya Bagamoyo yenye lengo la kuimarisha ukaguzi wa shule; na

c) uligharimia watumishi **36** wa Wakala katika mafunzo ya muda mfupi kuhusu matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za taaluma.

***Tume ya Taifa ya UNESCO***

26. **Mheshimiwa Spika,** Tume ina majukumu ya kutekeleza programu za UNESCO nchini kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari. Katika mwaka 2014/15, *Tume ya Taifa ya UNESCO*, ilitekeleza yafuatayo:

a) ilipitia utekelezaji wa Elimu kwa Wote 'EFA' kwa miaka 15 iliyopita na

kushirikisha wadau kuandaa agenda ya uelekeo wa Elimu nchini baada ya mwaka 2015;

b) iliwezesha na kuratibu mafunzo kwa wadau wanaoishi katika maeneo tengefu jinsi ya kuandaa miradi ya biashara kwa lengo la kuwajengea uwezo ili kutokutegemea kwa kiwango kikubwa mazao yapatikanayo kwenye maeneo tengefu;

c) iliandaa ripoti ya kazi zilizofanyika zinazoakisi hali ya uhifadhi wa maeneo yaliyo katika Urithi wa Dunia na kuziwasilisha katika kituo cha Urithi wa Dunia (UNESCO World Heritage Center);

d) iliandaa ripoti ya hali ya uhifadhi wa maeneo ya Tanzania yaliyoorodheshwa kwenye orodha ya Urithi wa Dunia ili kutathmini utekelezwaji wa mkataba wa UNESCO wa mwaka 1972; na

e) ilifadhili ukarabati wa Shule ya Msingi Magore ambayo iliharibika kwa mafuriko kwa kugharimia ununuzi wa madawati **170** yenye uwezo wa kukaa wanafunzi **680**, vitabu vya kiada kwa masomo yote kuanzia Darasa la I mpaka la VII kwa uwiano wa 1:1 kwa wanafunzi wote wa shule, seti moja ya komputa, printa na kinakilishi (photocopier), ujenzi wa

darasa moja na ofisi ya walimu pamoja na viti **20** na meza **20** kwa walimu wote.

## ***Baraza la Mitihani la Tanzania***

27. **Mheshimiwa Spika**, Baraza lina jukumu la kuendesha mitihani ya kuhitimu Elimu ya Msingi, Sekondari, Ualimu ngazi ya Astashahada na Stashahada na mtihani wa Maarifa na kusimamia uendeshaji wa mitihani itolewayo na bodi za nje ya nchi. Katika mwaka 2014/15, *Baraza la Mitihani la Tanzania,* lilitekeleza yafuatayo:

a) lilitahini wanafunzi waliomaliza: Elimu ya Msingi darasa la VII **808,085** na ufaulu kuongezeka toka asilimia **50.6** hadi asilimia **56.99%;** Elimu ya Sekondari kidato cha IV – **288,247** ambapo ufaulu uliongezeka toka asilimia **57.09** hadi asilimia **68.33.** Pia Baraza limeendesha mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa **12,316**;

b) lilisajili watahiniwa **14,718** wa mtihani wa Maarifa, watahiniwa **40,758** wa mtihani wa kidato cha sita na watahiniwa **19,766** wa mtihani wa ualimu;

c) liliendeleza ujenzi wa kituo cha Hazina Data kwa ajili ya kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu na taarifa za mitihani;

d) liliandaa, kuchapa na kusambaza vitabu vya Uchambuzi na tathmini ya mitihani ya taifa ya mwaka 2013 kama ifuatavyo: vitabu **86,650** kwa Darasa la VII, vitabu **21,712** kwa Kidato cha 4, vitabu **7,030** kwa Kidato cha 6. Aidha uchapaji wa vitabu vya Uchambuzi wa mitihani ya mwaka 2014 unaendelea; na

e) lilianza upembuzi yakinifu wa uandikishaji wa wanafunzi na kuwapa namba ambayo itatumika kuwatambua katika harakati zao kielimu na mafunzo kadri wanavyoendelea. Hili litafanywa kwa kushirikiana na kushauriana na NIDA.

***Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi***

28. **Mheshimiwa Spika,** Baraza lina majukumu ya kusimamia na kuratibu mitaala, ubora wa mafunzo, mitihani, tuzo, usajili na ithibati za vyuo vya elimu ya ufundi vya umma na binafsi nchini. Katika mwaka 2014/15, *Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi* lilitekeleza yafuatayo:

a) lilikagua Vyuo vya ufundi **114** na kutoa ushauri kuhusu usajili, ithibati na udhibiti wa ubora wa elimu ambapo: vyuo vya ufundi **89** vimesajiliwa kati

yake **47** vya ualimu na **42** visivyo vya ualimu; vyuo **18** vimepatiwa ithibati kati yake vitano **(5)** ni vya Sayansi na Teknolojia Shirikishi, kumi **(10)** vya Biashara, Utalii na Mipango na vitatu **(3)** vya Afya na Sayansi Shirikishi;

b) lilisajili wakufunzi **322** kati ya **467** sawa na asilimia **80.5** ya walioomba usajili;

c) liliratibu udahili wa wanafunzi **44,271** (Wanawake **15,428** na Wanaume **28,843**) katika vyuo vya ufundi; kati yao **27,878** ni wa ngazi ya Astashahada na Stashahada, na **16,393** (Wanawake **6,980** na Wanaume **9,413**) ngazi ya Shahada;

d) liliidhinisha mitaala 10 ya kitaifa, mitaala 60 ya vyuo vya ufundi katika programu za Sayansi na Teknolojia Shirikishi, Biashara, Utalii na Mipango Afya na Sayansi Shirikishi na Elimu, Ufundishaji na Ujifunzaji na kuratibu mafunzo kwa walimu 195 ya jinsi ya kutumia mitaala inayozingatia umahiri; na

e) lilivijengea uwezo wa kutengeneza mfumo wa uhakiki ubora wa mafunzo Vyuo 22; kati ya hivyo, vyuo vitano

**(5)** vimetengeneza mfumo wa uhakiki ubora wa mafunzo na kuwezesha Idara zake kutambuliwa na kupatiwa ithibati.

***Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere***

29. **Mheshimiwa Spika,** Chuo kina majukumu ya kuendesha mafunzo katika fani za Sayansi za Jamii; kutoa mafunzo ya uongozi; kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta ya umma na binafsi. Katika mwaka 2014/15, *Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,* kilitekeleza yafuatayo:

a) kilidahili jumla ya wanafunzi **841** kati yao wanafunzi **229** wa programu za Astashahada, **276** wa programu za Stashahada na **336** wa programu za Shahada ya Kwanza;

b) kilianzisha mafunzo katika fani za Menejimenti ya Rasilimaliwatu (Human Resource Management) na Maendeleo ya Uchumi (Economic Development) ambapo Jumla ya wanafunzi **196** wamedahiliwa katika programu za: Rasilimaliwatu - Astashahada **97** na Stashahada **38**, Maendeleo ya Uchumi - Astashahada **44** na Stashahada **17**;

c) kilianzisha kozi mpya ya Uongozi na Maadili ambayo ilizinduliwa na Rais Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 13 Aprili 2015 ili kusaidia Taifa katika harakati zake za kuwajenga viongozi na Watanzania kwa ujumla katika maadili na utawala bora;

d) kiligharimia mafunzo kwa wahadhiri wanane (8) katika ngazi ya uzamili watano (5) na uzamivu watatu (3) ili kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi na kuajiri wahadhiri wapya 25 kwa lengo la kuimarisha ufundishaji; na

e) kiliendeleza ujenzi wa hosteli katika kampasi ya Kivukoni ambapo kazi za kuezeka, kuweka milango ya ndani na sakafu zimekamilika.

***Chuo cha Ufundi Arusha***

30. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kina majukumu ya kutoa elimu ya ufundi katika fani za magari, ujenzi, umwagiliaji, mitambo, umeme, barabara, sayansi na teknolojia ya maabara, eletroniki na mawasiliano ya anga; kwa kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada katika ujenzi na umwagiliaji; kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma. Katika mwaka 2014/15, *Chuo cha Ufundi Arusha*

kilitekeleza yafuatayo:

a) kilidahili wanafunzi **600** wa mwaka wa kwanza (**570** wa ngazi ya Astashahada na **30** wa ngazi ya Shahada);

b) kilianza mchakato wa kuhuisha mitaala 6 ya programu zilizopo za Ufundi Sanifu (NTA 4-6) kwa lengo la kuzalisha wataalamu wanaoendana na mahitaji ya soko la ajira;

c) kiliongeza udahili wa wanafunzi wa kike wenye sifa pungufu kwa kutoa kozi ya awali (*Pre-Entry Course*) ya kujiunga na chuo kwa kushirikiana na Mfuko wa Elimu Tanzania (TEA) ambapo jumla ya wanafunzi **126** wa kike walijiunga na chuo kwa utaratibu huo;

d) kiliajiri wakufunzi **27** na kugharimia mafunzo ya wakufunzi **15**;

e) kilikamilisha rasimu ya mitaala ya program ya stashahada ya Ualimu wa masomo ya Sayansi na stashahada ya Ufundi Sanifu (NTA 4-6) katika fani ya Magari na Mitambo Mikubwa na kuiwasilisha NACTE kwa ajili ya kupata ithibati;

f) kilikamilisha Mpango Mkakati wa kuanzisha kituo cha kuzalisha umeme cha Kikuletwa. Upembuzi yakinifu kwa ajili ya ukarabati wa kituo umeanza;

g) kiliendeleza ujenzi wa jengo la Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji na kufikia asilimia **99**; na

h) kilifanya utafiti wa chanzo cha umeme wa maji Wilayani Mbulu, na kutoa Ushauri elekezi wa miradi ya maji kutoka mlima Meru kwenda Wilayani Longido na kutoka chanzo cha maji cha West Kilimanjaro-mto Samba kwenda Wilayani Longido.

***Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi***

31. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ina majukumu ya kuratibu, kudhibiti, kugharimia, kutoa na kukuza mafunzo ya ufundi stadi nchini. Katika mwaka 2014/15, *Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi*, ilitekeleza yafuatayo:

a) ilianza maandalizi ya awali ya ujenzi wa vyuo vitano (5) vya Wilaya za Kilindi, Namtumbo, Ludewa, Ukerewe na Chunya pamoja na vyuo 4 vya Mikoa

ya Geita, Simiyu, Rukwa na Njombe;

b) ilikarabati karakana za vyuo vya Moshi,Tanga, Mwanza na Kihonda. Aidha, imeteua Mtaalamu Elekezi kwa ajili ya ujenzi wa mitandao ya TEHAMA katika vituo vya VETA vya Oljoro - Arusha, Dakawa - Morogoro, Singida, Ulyankulu - Tabora;

c) ilikamilisha miongozo ya kutambua na kurasimisha ujuzi wa Ufundi Stadi uliopatikana katika mfumo wa mafunzo usio rasmi na kufanya majaribio katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Morogoro na Mwanza ambapo Vijana **144** kati ya **201** waliotahiniwa walikidhi viwango na kupatiwa vyeti ngazi ya kwanza ya ufundi stadi katika fani za useremala, uashi, ufundi magari na mapishi;

d) ilikamilisha taratibu za kupata fedha kupitia Mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika mikoa mipya ya Geita, Simiyu, Njombe na Rukwa. Taratibu za upatikanaji wa washauri elekezi kwa ajili ya kuandaa makabrasha ya ujenzi wa vyuo husika zinaendelea. Vilevile serikali imepata

ufadhili kutoka serikali ya China kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha mkoa wa Kagera. Eneo lenye ukubwa wa hekta **40.53** limetolewa na wanakijiji wa Burugo kata ya Nyakato; na

e) iliendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi **171** (wanaume **96** na wanawake **75**) kutoka makampuni **10**. Aidha, washiriki **981** (wanaume **369** na wanawake **612**) kutoka sekta isiyo rasmi wamepatiwa mafunzo katika stadi mbalimbali.

***Mamlaka ya Elimu Tanzania***

32. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ina majukumu ya kutafuta na kubaini vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kugharimia maendeleo ya sekta ya elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wadau wa elimu kuchangia kwa hiari katika miradi ya elimu. Katika mwaka 2014/15, *Mamlaka ya Elimu Tanzania*, ilitekeleza yafuatayo:

a) iligharimia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya elimu iliyo katika mikakati ya mpango wa Matokeo Makubwa Sasa;

b) iligharimia mafunzo ya '*Pre-entry'* kwa wanafunzi wa kike **265** ili kuwawezesha

kupata sifa stahiki za kujiunga na vyuo vya elimu ya ufundi nchini;

c) iliandaa maandiko **15** na kuyawasilisha kwa wafadhili mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabenki, mashirika ya misaada ndani na nje ya nchi. Jumla ya fedha na vifaa vyenye thamani ya shilingi Milioni **571** vimepatikana kupitia maandiko hayo; na

d) iligharimia ujenzi wa Hosteli ya wanafunzi wa kike katika shule ya sekondari Kibaigwa, Wilaya ya Kongwa ambapo ujenzi uko katika hatua za uwekaji paa na umaliziaji. Aidha, Ujenzi wa Hosteli za wanafunzi wa kike katika shule ya sekondari Ufana, Wilaya ya Babati na shule ya sekondari Mibukwe, Wilaya ya Bumbuli uko katika hatua ya mchakato wa kutafuta wakandarasi wa ujenzi wa hosteli hizo.

## ***Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania***

33. **Mheshimiwa Spika,** Tume ina majukumu makuu ya kusimamia ubora wa Elimu ya Juu, kutoa ithibati, kuratibu uanzishwaji wa Vyuo Vikuu, na kuidhinisha programu zinazofundishwa ili zikidhi maendeleo ya Taifa na soko la ajira. Katika mwaka

2014/15, *Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania*, ilitekeleza yafuatayo:

a) iliratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi **59,887** (Wanawake **21,059** na Wanaume **38,828**) katika Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki nchini sawa na asilimia **99.8** ya lengo;

b) ilifanya tathmini ya mpango wa uanzishaji/uhuishaji wa vyuo sita **(6)** ambapo: Chuo Kikuu cha Ardhi na Chuo Kikuu Kishiriki cha Stella Maris, Mtwara vilipewa ithibati ya kuendelea kutoa mafunzo; Chuo Kikuu Kishiriki cha Mtakatifu Agostino Marian, Bagamoyo kilipata usajili wa muda; Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kilipata usajili wa kudumu; na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara, Moshi, Chuo Kikuu cha Kikatoliki, Mwenge na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ruaha vilipandishwa hadhi kuwa vyuo vikuu kamili;

c) iliimarisha mfumo wa udahili wa pamoja wa wanafunzi wa Elimu ya Juu na kuweza kupokea maombi ya wahitimu wa: Kidato cha Sita na Stashahada, wenye vyeti vya kigeni na

wenye sifa nyinginezo (Recognition of Prior Learning);

d) ilitathmini na kuidhinisha programu **17** za masomo katika vyuo vikuu sita **(6);**

e) iliratibu upatikanaji wa wanataaluma **17** kutoka Vyuo Vikuu nchini waliojiunga na Masomo ya Uzamivu chini ya makubaliano ya Serikali ya Tanzania na Ujerumani (Deutscher Akademischer Austauch Diest - DAAD);

f) iliratibu na kuandaa Maonyesho ya Tisa ya Elimu ya Juu , Sayansi na Teknolojia ambapo kumekuwepo ongezeko la washiriki kutoka taasisi za nje zikiwemo za China, Uingereza, Marekani, Malaysia, Afrika Kusini, Zimbabwe, Dubai, Kenya, Uganda na Uturuki; na

g) iliandaa Kongamano la Elimu ya Juu ambalo kila mwaka hujadili masuala mbalimbali ya elimu kwa ujumla ili

kubaini changamoto mbalimbali na jinsi ya kukabiliana nazo.

***Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu***

34. **Mheshimiwa Spika**, Bodi hii ina majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi raia wa Tanzania wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi na kukusanya marejesho ya mikopo hiyo. Katika mwaka 2014/15, *Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu*, ilitekeleza yafuatayo:

a) ilitoa mikopo kwa wanafunzi **99,590** wakiwemo **2,117** wa Stashahada ya Elimu ya Ualimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati na hivyo kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Juu;

b) ilitoa ruzuku kwa Wanafunzi **1,793** sawa na asilimia **94.3** ya lengo wanaosomea Shahada za Udaktari wa Binadamu, Meno na Mifugo katika vyuo vya elimu ya Juu;

c) ilikusanya marejesho ya mikopo kiasi cha shilingi **15,978,993,320.04** sawa na asilimia **45.5** ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2014/15 na hivyo kufikia shilingi **75,575,793,215**

sawa na asilimia **45.45** ya shilingi **165,008,246,475** za madeni yaliyoiva;

d) iliendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma kwa njia ya magazeti, redio na televisheni kuhusu dhana ya uchangiaji, taratibu za utoaji mikopo pamoja na urejeshwaji wake na wajibu wa kila mdau kuchangia Elimu ya Juu; na

e) iliendelea kuimarisha ofisi za kanda kwa kununua magari mawili (**2)** na kuyapeleka kwenye ofisi za kanda. Aidha, iliendelea kuunganisha ofisi za kanda kwenye mtandao wa mawasiliano wa Bodi.

***Chuo Kikuu cha Dar es Salaam***

35. **Mheshimiwa Spika,** Chuo hiki kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo mbalimbali ya elimu na mafunzo. Katika mwaka 2014/15, *Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* kilitekeleza yafuatayo:

a) kilidahili wanafunzi **7,252** wa Shahada ya kwanza (wanaume **4,667**, wanawake **2,585**), **1,653** wa shahada za uzamili (wanawake wakiwa **41%**) ambapo **151**

ni wa shahada ya uzamivu. Aidha, kilianzisha Shule kuu ya Sayansi za Afya na Koleji ya Sayansi za Kilimo na Teknolojia za Uvuvi kwa lengo la kuziba pengo la utaalamu na ujasiriamali ili kukuza uchumi wa nchi;

b) kiliendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake ikiwa ni pamoja na wanataaluma katika ngazi ya shahada za uzamili na wafanyakazi waendeshaji katika maeneo ya uongozi, udhibiti wa ubora, rasilimaliwatu, ununuzi wa umma, utunzaji wa nyaraka na mipango;

c) kilikamilisha ujenzi wa madarasa, maabara na miundombinu mingine (majengo 7 ya ghorofa na madogo 3), na kuanza mchakato wa ununuzi wa vifaa vya maabara za sayansi na maktaba zilizofadhiliwa na serikali kupitia mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

d) kilikamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa nne la Shule Kuu ya Biashara ambalo limejengwa kwa fedha za ndani na kuendeleza ujenzi wa shule mpya ya msingi ya mazoezi yenye viwango vya kimataifa kwa kushirikiana na Serikali

ya Watu wa China; na

e) kimeanzisha utaratibu wa kuwa na vituo vya utafiti na wiki ya utafiti ambapo tafiti mbalimbali huoneshwa kwa jamii na kushindanishwa ili kukuza maarifa na uchumi wa nchi.

***Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam***

36. **Mheshimwa Spika**, Chuo hiki ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu. Katika mwaka 2014/15, *Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam* kilitekeleza yafuatayo:

a) kilidahili wanafunzi **1,700** katika fani mbalimbali za elimu kati ya hao wanafunzi **310** ni wa fani ya sayansi;

b) kiliendelea kufanya usanifu kwa ajili ya ukarabati wa jengo la kitivo cha humanitia na sayansi ya jamii na jengo la Utawala. Aidha, kiendeleza ujenzi wa maabara ya sayansi, madarasa na kituo cha taaluma za utangazaji kupitia mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu;

c) kilinunua aina **134** za Kemikali za maabara na vinasa sauti – 'tape recorder' kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;

d) kiligharamia wahadhiri **74** katika mafunzo ngazi ya shahada za uzamili na **11** shahada za uzamivu ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo na kuongeza ufanisi; na

e) kiliajiri wafanyakazi **10** kujaza nafasi zilizoachwa wazi, kati yao sita (**6)** ni walimu na wanne (**4)** waendeshaji.

***Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa***

37. **Mheshimiwa Spika,** Chuo hiki ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu. Katika mwaka 2014/15, *Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa* kilitekeleza yafuatayo:

a) kilidahili wanafunzi **1,284** ngazi ya shahada (wanawake **325** na wanaume **959**) sawa na asilimia **107** ya lengo;

b) kiliendeleza ujenzi wa maabara ya sayansi, madarasa na kituo cha taaluma za utangazaji kupitia mradi wa

Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu; na

c) kiligharimia mafunzo kwa wahadhiri **16** kati yao wanawake **3** katika viwango vya shahada za uzamili **1** na uzamivu **15** kupitia wafadhili mbalimbali.

***Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo***

38. **Mheshimiwa Spika,** Chuo hiki kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za kilimo, mifugo, mazingira na maendeleo kwa ujumla. Katika mwaka 2014/15, *Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo* kilitekeleza yafuatayo:

a) kilianzisha programu 2 za mafunzo ngazi ya Shahada ya Uzamili (Msc in Health of Aquatic Resources na Msc in Agricultural Statistics) na Programu 1 ngazi ya Stashahada (Diploma in Laboratory Science and Technology);

b) kilikamilisha ujenzi wa majengo manne (4) yaliyogharimiwa na mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na kuongeza uwezo wa Chuo kudahili wanafunzi **800** zaidi;

c) kiliendeleza Ujenzi wa Maabara kubwa ya Kitivo cha Sayansi inayogharamiwa

na 'Enhancing Pro –Poor Innovation for Natural Resources and Agricultural Value Chains' (EPINAV); na

d) kiliendeleza ujenzi wa jengo la kufundishia kwa ufadhili wa Norway (CCIAM) hadi kufika asilimia **99** na kuanza ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kulaza wanafunzi **40** katika Kampasi ya Olmotonyi.

***Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi***

39. **Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Chuo hiki kilichokuwa kinalelewa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kimepandishwa hadhi na kuwa Chuo Kikuu kamili ambapo sasa kinajulikana kama Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (Moshi Cooperative University – MOCU) kikiwa na tawi moja kule Kizumbi Shinyanga. Chuo kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za ushirika, maendeleo ya jamii, biashara, oganaizesheni, ujasiriamali na masuala mtambuka. Katika mwaka 2014/15, *Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi,* kilitekeleza yafuatayo:

a) kilidahili wanafunzi **4,122** na kutoa wahitimu **2,193** katika ngazi ya Astashahada hadi Uzamili;

b) kiligharimia mafunzo ya watumishi **63** wakiwemo **1** Astashahada, **1** Shahada ya kwanza, **28** Uzamili na **33** Uzamivu. Aidha, kati yao **13** wamehitimu mwaka 2014 wakiwamo **1** Stashahada, **9** Uzamili na **3** Uzamivu;

c) kiliboresha programu za utafiti kwa kushindanisha maandiko ili kupata ufadhili kupitia mfuko wa chuo "Small Scale Competetive Research Grants" ambapo tafiti **18** zimefanyika katika maeneo ya Ushirika, "Micro Finance na Menejimenti";

d) kilitoa elimu kwa kuchapisha na kusambaza Jarida la Utafiti (Research Report Series) na Jarida la Ushirika na Biashara (Journal of Co-operative and Business Studies). Aidha, usambazaji ulifanyika kwa kupitia Makongamano, Maonesho, Warsha na Semina;

e) kilikarabati ofisi katika kituo cha Dodoma;

f) kiliwajengea uwezo watafiti **50** wa Chuo kwa kushirikiana na vyuo vya nje ya nchi hususani Chuo Cha Ushirika cha Uingereza, Chuo Kikuu cha Stirling cha Uingereza, Chuo Kikuu cha Malawi, Chuo Kikuu cha Makerere, Chuo Kikuu

cha Zambia na "Humber Institute of Technology and Advanced Learning (HITAL)"; na

g) kupitia Taasisi ya Elimu Endelevu ya Ushirika kiliratibu mafunzo ya Ushirika kwa wadau **11,841** wakiwemo wanaume **7,416** na wanawake **4,825**, kuandaa na kurusha vipindi vya redio kuhusu elimu ya ushirika kupitia Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) kila jumapili na kuandaa na kuhariri masomo ya ushirika kwa njia ya posta kwa wanafunzi **118** wakiwemo wanaume **68** na wanawake **50**).

***<u>Chuo Kikuu Huria cha Tanzania</u>***

40. **Mheshimiwa Spika,** Chuo kina majukumu ya kutoa Elimu ya Juu kwa njia ya Masafa na Ana kwa Ana; kutafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kueneza maarifa kupitia vituo vyake vilivyopo mikoani. Katika mwaka 2014/15, *Chuo Kikuu Huria cha Tanzania* kilitekeleza yafuatayo:

a) kilidahili Wanafunzi **10,290** wakiwemo **3,336** wa Astashahada na Stashahada, **3,793** wa Shahada ya kwanza, **3,064** wa Shahada ya Uzamili na **97** wa Shahada ya Uzamivu;

b) kilikamilisha ujenzi wa maabara ya

kompyuta katika vituo vya mikoa ya Mtwara na Mara pamoja na kuweka kompyuta katika maabara ya mkoa wa Mtwara;

c) kiliweka mfumo wa intaneti isiyotumia waya (wireless internet) katika mikoa ya Dodoma, Lindi, Mtwara, Mara, Njombe na Tabora;

d) kilikamilisha michoro sanifu (architectural design) wa majengo ya maabara ya Sayansi (Science Multi-purpose Lab) na jengo la madarasa makao makuu ya chuo Bungo Kibaha; na

e) kilikarabati majengo katika vituo vya mikoa ya Kagera, Mtwara, Ruvuma, Temeke, Makao Makuu ya kudumu ya Chuo Bungo Kibaha, Makao Makuu ya muda ya Chuo Kinondoni na kituo cha uratibu cha Kibungo nchini Rwanda.

***Chuo Kikuu Ardhi***

41. **Mheshimiwa Spika,** Chuo hiki kina majukumu ya kutoa mafunzo, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika nyanja za maendeleo ya ardhi, nyumba, mazingira na ujenzi. Katika mwaka 2014/15, *Chuo Kikuu Ardhi*

kilitekeleza yafuatayo:

a) kilidahili wanafunzi **3,871** wakiwemo wanawake **1,386** na wanaume **2,485** sawa na asilimia 93.5 ya lengo katika programu mbalimbali za chuo;

b) kiligharimia mafunzo ya watumishi **86** wakiwemo **1** Astashahada, **9** Stashahada, **9** Shahada ya kwanza, **24** Uzamili na **43** Uzamivu;

c) kiliendelea na ujenzi wa jengo la 'Lands Building' ambapo ofisi **21** zenye nafasi ya kutosha wanataaluma **50** zimekamilika;

d) kilifanya tafiti **34** katika maeneo ya mabadiliko ya tabia ya Nchi, hali ya hewa na matumizi ya ardhi, hali ya hewa na usalama wa chakula, uchafuzi wa mazingira kupitia shughuli za kilimo na usafirishaji, jinsia na ufahamu juu ya maambukizi ya magonjwa yanayotokana na kujamiiana, usanifu wa majengo, urasimishaji makazi na mchango wake katika kuondoa umasikini, usimamizi wa mazingira na udhibiti wa hewa ukaa na upimaji ardhi na taarifa za kijiografia zinazosaidia wakulima wadogo wa kahawa. Aidha, Machapisho ya taarifa za tafiti **28**

yameandaliwa na kusambazwa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI; Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Majiji na Manispaa za Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Tanga, Kinondoni, Ilala, Temeke na Zanzibar, SUA, SIDA, CCIAM na Benki ya Dunia;

e) kilitoa ushauri wa kitaalamu kupitia miradi sita (**6)** ya 'Tanzania Cities Network' unaohusisha Miji, Manispaa na Majiji tisa **(9)** ya Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Tanga, Kinondoni, Temeke, Ilala na Zanzibar; na

f) kilikarabati miundombinu katika mabweni matano (**5),** kununua samani kwa ajili ya matumizi ya hosteli, kutayarisha mchoro kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha wanafunzi (Students Centre) pamoja na kutoa huduma ya ushauri nasaha kwa wanafunzi **190**.

## ***Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili***

42. **Mheshimiwa Spika,** Chuo hiki kina majukumu ya kutoa mafunzo, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu

katika maeneo ya tiba na afya ya binadamu. Katika mwaka wa 2014/15, *Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili* kilitekeleza yafuatayo:

a) kilizalisha wataalam **952** wakiwemo wa Stashahada **371**, Stashahada ya Juu **12**, Shahada ya kwanza **372**, Shahada za Uzamili **196**, na Shahada ya Uzamivu **1** katika fani za afya za Madaktari, Wafamasia, Wataalamu wa Maabara, Elimu ya Afya kwa Umma na Wauguzi;

b) kiliendelea na ujenzi wa jengo la Kituo cha Mafunzo ya Elimu ya Fani za Afya (Centre for Health Profession Education). Aidha, kiliendelea na ujenzi wa Hospitali ya Kufundishia ya Kampasi ya Mloganzila unaotarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2016 ambapo: umeme umekwisha fika eneo la mradi, ujenzi wa barabara kutoka Barabara kuu ya kwenda Morogoro umekamilika kwa kiwango cha lami, usimikaji wa miundombinu ya maji kupitia DAWASCO unaendelea, taratibu za kununua na kusimika (installation) vifaa tiba umeanza; na

c) kilikamilisha utafiti kuhusu VVU

kupitia mradi wa TaMoVac-0I ambapo matokeo yalionesha kwamba chanjo ya majaribio ni salama na yaweza kutolewa kwa njia rahisi kuliko ilivyokuwa awali. Aidha, kiliendeleza utafiti kuhusu VVU kupitia mradi wa TaMovac II uliohusisha nchi za Tanzania na Msumbiji. Utafiti unaendelea vizuri na unategemewa kumalizika tarehe 30 Juni 2015. Vilevile chuo kiliendeleza utafiti kuhusu ugonjwa wa Malaria.

d) kilifanya ukarabati katika hosteli za wanafunzi zilizopo barabara ya Chole, Masaki.

***Chuo Kikuu Mzumbe***

43. **Mheshimiwa Spika,** Chuo hiki kina majukumu ya kutoa mafunzo, kutafiti na kutoa ushauri katika maeneo ya maarifa na stadi za menejimenti. Katika mwaka 2014/15, *Chuo Kikuu Mzumbe* kilitekeleza yafuatayo:

a) kilidahili wanafunzi **4,815** wakiwemo **255** katika programu za Astashahada, **393** Stashahada, **2,587** Shahada ya kwanza, **1,566,** Shahada ya uzamili na **45** Shahada ya Uzamivu;

b) kiligharimia mafunzo ya watumishi **12** katika mafunzo ya shahada ya uzamili na **5** shahada ya uzamivu; na

c) kiliimarisha masuala ya menejimenti, uongozi na sayansi ya jamii kwa kukamilisha tafiti katika maeneo **6** na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo **18** pamoja na kuchapisha vitabu **10** na machapisho **123**.

***<u>Chuo Kikuu cha Dodoma</u>***

44. **Mheshimiwa Spika,** Chuo hiki kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya Elimu ya juu. Katika mwaka 2014/15, *Chuo Kikuu cha Dodoma* kilitekeleza yafuatayo:

a) kilidahili wanafunzi **9,550** wakiwemo **79** astashahada, **2,678** stashahada, **6,349** shahada ya kwanza, **400** shahada ya uzamili na **44** shahada ya uzamivu;

b) kiliendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji safi na maji taka kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma (DUWASA) ambapo, matanki mawili

kati ya matatu ya kuhifadhia maji yenye uwezo wa kuhifadhi lita **8,000** za maji yamekamilika, Mabomba yameanza kutandazwa kwenye njia za usambazaji wa maji zenye urefu wa kilomita **14.28** na ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhia maji taka unaendelea; na

c) kilifanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam kwa ushirikiano na Taasisi mbalimbali nje na ndani ya nchi zikiwemo (ASARECA, CIDA, COSTECH, EAAP, IITA ICURA, VICRES, TCRA, REPOA, VLIR, WOTRO) ambapo, miradi **10** ya utafiti inaendelea, miradi minne **(4)** imekamilika, miradi mitano **(5)** mipya imeanzishwa na miradi minane **(8)** iko katika hatua za mapendekezo

***Usimamizi na Utekelezaji wa Programu na Miradi***

45. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/15, Wizara yangu ilitekeleza miradi mbalimbali kama ifuatayo:

a) iliendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za elimu na mafunzo ambapo:

i) kupitia Mpango wa Maendeleo ya

Elimu ya Sekondari (MMES II) walimu wawezeshaji 254 na walimu **540** wamepewa mafunzo ya matumizi ya TEHAMA katika kutoa mafunzo;

ii) kupitia mradi wa E-Education for Secondary Schools TZ Mainland Serikali inaendelea kuwasiliana na serikali ya China kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuzijengea uwezo shule **150;**

iii) kupitia mradi wa STHEP programu ya kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi katika shule za sekondari kwa kutumia TEHAMA imeanza kutekelezwa kwa majaribio ambapo: moduli za kidigitali (Digital) za mada ngumu **15** zimeandaliwa, Walimu **2,000** wamebainishwa kwa ajili ya kujengewa uwezo na Vyuo Vikuu vitano vinaendelea kujengewa uwezo ili kuendesha mafunzo hayo; na

b) iliimarisha mfumo wa upatikanaji na utoaji wa taarifa za elimu (Education Sector Management Information System - ESMIS) katika ngazi zote na kuhifadhi taarifa na takwimu katika ofisi za Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA). Shule/vyuo na taasisi za elimu

kwa sasa zinaweza kuingiza takwimu zao moja kwa moja kwa kutumia namba zao za siri. Aidha, Takwimu za shule/vyuo kwa mwaka 2014 zimeandaliwa kwa ngazi ya shule/chuo; na

c) iliendelea kutegemeza utoaji wa elimu ya msingi nchini kupitia Mpango wa “LANES”. Huu ni Mpango wa Kitaifa wa Kukuza stadi za Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu kwa watoto wa umri kati ya miaka mitano **(5)** hadi kumi na tatu **(13)**, walio shuleni darasa la kwanza **(1)** hadi la nne **(4)** na wale walio nje ya mfumo rasmi miaka tisa **(9)** hadi kumi na tatu **(13)**. Katika mwaka 2014/15, walimu wa darasa la I na II wapatao **13,788** pamoja na walimu **925** wa Elimu ya Watu Wazima wako katika mafunzo yanayotarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015.

d) iliendelea kutegemeza utoaji wa elimu ya sekondari kama ifuatavyo:

   i. iliwapatia mafunzo kazini walimu **6,555** wa masomo ya Hisabati, Sayansi na Lugha (Kiswahili na English);

   ii. iliwezesha kukamilisha miundombinu katika shule **162** za awamu ya kwanza na kufanya jumla ya

shule zilizokamilika kuwa **217** kati ya **264** za awamu ya kwanza;

iii. Vyuo **6** vya ualimu Klerruu, Morogoro, Butimba, Monduli, Tukuyu, na Songea vimepatiwa vifaa na kemikali kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa walimu tarajali; na

iv. iliendesha mafunzo ya "bridging course" kwa wahitimu **240** wa kidato cha sita wa masomo ya sayansi katika chuo cha ualimu Monduli.

e) iliingia makubaliano na Serikali ya Canada kupitia Umoja wa Vyuo vya Ufundi na Taasisi nchini Canada (CICan) katika kutekeleza Mpango wa Kuongeza Ujuzi wa Kuweza Kuajiriwa/ Kujiajiri (Improving Skills Training for Employment Program-ISTEP) 2014-2019 kwa Watanzania **1,200** katika Sekta za Utalii, Gesi Asilia, Mafuta na Madini.

f) iliendelea kufanya tafiti ili kukamilisha mradi wa Education and Skills for Productive Jobs ambao utakuwa ni

mwendelezo wa mradi wa STHEP ambao unakwisha ifikapo Januari 2016;

g) iliunda Kamati ya kuandaa utekelezaji wa mradi wa Partnership for Applied Science, Engineering and Technology (PASET) katika ngazi ya taifa; na

h) ilianzisha taratibu za kujiunga na mradi wa African Centres of Exellence unaolenga kuwa na vituo mahiri vya utafiti vya kikanda katika baadhi ya vyuo vikuu nchini.

***<u>Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa</u>***

46. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kwa kushirikiana na OWM TAMISEMI ilitekeleza mikakati ya matokeo makubwa sasa. Kwa mujibu wa taarifa ya mwaka mmoja (2013/14) sekta ya elimu imefanikiwa kwa asilimia **81** na kushika nafasi ya kwanza katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mikakati hiyo. Mafanikio ambayo tayari yamehakikiwa na 'Presidential Delivery Bureau' ni kama yafuatayo:

a) kupitia Baraza la Mitihani Tanzania kwa mara ya kwanza shule zilipangwa kulingana na ufaulu kwa lengo la kuifahamisha jamii kuhusu ufaulu

wa shule kwa makundi. Taarifa hii ilitolewa kwenye mitandao na vitabu;

b) kutoa tuzo kwa shule na wanafunzi waliofanya vizuri kwenye matokeo ya mitihani ya darasa la saba na kidato cha IV. Jumla ya tuzo **3,044** zilitolewa kwa shule zilizopata ufaulu uliotukuka na zile zilizopanda kwa ufaulu ikilinganishwa na mwaka 2013. Zawadi hizi zilitolewa kwenye maadhimisho ya Wiki ya Elimu yaliyofanyika mwezi Mei, 2014;

c) tathmini ya uwezo wa wanafunzi kujua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) ilifanyika mwezi Novemba, 2013 kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID). Tathmini ilijumuisha shule za msingi **200** na wanafunzi **2,226** na matokeo yake yatasaidia kuinua ubora wa ujifunzaji na ufundishaji wa Stadi hizo shuleni;

d) kiongozi cha Kuimarisha Utendaji wa Shule (School Improvement Toolkit) kiliandaliwa na wakuu wa shule **2,982** walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kusimamia elimu;

e) walimu **4,103** wa masomo ya Sayansi,

Hisabati na Lugha (Kiswahili na English) walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kutambua wanafunzi wenye uwezo mdogo wa kumudu masomo. Shule **1,325** ziliendesha mafunzo rekebishi kwa wanafunzi waliotambuliwa na kuwajengea uwezo wa kumudu masomo yao vema;

f) ujenzi wa miundombinu ya shule **47** za Sekondari kati ya **264** zilizolengwa katika awamu ya kwanza ulikamilika. Lengo ni kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya shule **1,200** katika awamu tatu.

g) madeni ya **Sh. 1,852,162,158.21** ya malimbikizo ya mishahara yalilipwa kwa watumishi **916** wa Wizara.

47. **Mheshimiwa Spika**, matokeo ya utekelezaji wa mikakati hii ni kupanda kwa ufaulu wa mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi (Darasa la Saba) kutoka asilimia **50.6** mwaka 2013 hadi kufikia asilimia **56.99** mwaka 2014 na kupanda kwa ufaulu wa mtihani wa kumaliza Elimu ya Sekondari (Kidato cha Nne) kutoka asilimia **50.09** mwaka 2013 hadi kufikia asilimia **68.33** mwaka 2014. Taarifa ya utekelezaji ya

Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa katika Elimu kwa upande wa TAMISEMI imeshatolewa na Mhe. Waziri Mkuu wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2014/15.

## IV. CHANGAMOTO

48. **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu na bajeti ya mwaka 2014/15, Wizara yangu ilipata changamoto katika maeneo mbalimbali inayoyasimamia kama ifuatavyo:

a) kuimarisha mifumo ya usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sera za elimu hususan katika maeneo yaliyoguswa na ugatuaji;

b) upatikanaji wa rasilimali fedha za kutosha na kwa wakati na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara yakiwemo:

- kulipa madeni ya wazabuni na huduma nyingine ambayo sasa yanafikia shilingi **45,855,370,632.7** ambapo shilingi **25,195,672,974.2** ni deni la wazabuni wa vyuo vikuu na vyuo vya ufundi na shilingi **5,148,207,930.00** ni deni la posho

za wahadhiri;

- kuwezesha upanuzi wa miundombinu ya elimu ya ufundi ili kukabiliana na mahitaji ya taifa katika fani za ufundi;

c) kupata walimu mahiri wa kufundisha stadi za KKK kwa kiwango cha kutosha kwa wanafunzi wa madarasa ya chini (Darasa la I na II);

d) namna ya kuongeza idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu ili ikaribiane na kupita ile ya nchi jirani ambazo zina kiwango cha wastani wa asilimia 5 wa rika lengwa ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.7 kwa Tanzania;

e) upatikanaji wa wataalam wa Kitanzania katika mnyororo wa thamani katika fani za gesi, mafuta, chuma, urani, makaa ya mawe na madini mengine; na

f) upatikanaji wa rasilimaliwatu na rasilimali nyingine za kutosha ili kuwezesha uthibiti wa ubora wa elimu na mafunzo kufanyika kwa ufanisi kulingana na miongozo ya uthibiti ubora katika ngazi zote.

49. **Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine zilizojitokeza ni hizi zifuatazo:

a) kuinua kiwango cha ufahamu, maarifa na ujuzi wa walimu wakufunzi na wahadhuri ili kuwa mahiri katika kutoa elimu na mafunzo yanayokidhi mahitaji ya jamii kulingana na mazingira na maendeleo ya nchi; upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika elimu na mafunzo mbalimbali na kuinua kiwango cha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

b) upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika elimu na mafunzo mbalimbali na kuinua kiwango cha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

c) kuinua kiwango cha walimu, wakufunzi na wahadhuri katika matumizi sahihi ya TEHAMA kama sehemu ya nyezo muhimu katika mafunzo;

d) ongezeko la gharama za kusomesha wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo;

e) ongezeko la mahitaji ya walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati katika ngazi zote za elimu na mafunzo;

f) uhaba mkubwa wa wakufunzi na wahadhiri katika vyuo vyetu ikiwemo

vyuo vya elimu ya juu; na

g) uhaba wa watumishi wenye sifa kuchaguliwa kuwa viongozi katika ngazi mbalimbali vyuoni, hususan vya elimu ya juu na ufundi.

50. **Mheshimiwa Spika,** changamoto hizi na nyingine budi zipewe ufumbuzi wa haraka kabla hazijaendelea kuwa kero kubwa katika azma yetu ya kupata taifa lenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

## V. VIPAUMBELE NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2015/16

51. **Mheshimiwa Spika,** vipaumbele vya sekta ya elimu vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Taifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2015/16 ni:

a) kuongeza upatikanaji wa fursa ya elimu kwa usawa katika ngazi zote za elimu na mafunzo;

b) kuinua ubora wa elimu na kujenga stadi stahiki katika ngazi zote za elimu na mafunzo; na

c) kuimarisha taasisi za usimamizi wa ubora wa elimu pamoja na ufuatiliaji na tathmini ili zitekeleze majukumu

ya kuhakikisha elimu bora inatolewa katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

52. **Mheshimiwa Spika,** kulingana na hati idhini iliyotolewa mwaka 2010, wizara yangu inalenga kutekeleza vipaumbele vya sekta katika maeneo yafuatayo:

    a) utungaji na utekelezaji wa Sera za Elimu;

    b) ithibati ya Shule;

    c) Uthibiti Ubora wa elimu;

    d) mafunzo ya Ualimu, hususan wa sayansi, hesabu, ufundi ikiwemo ufundi sanifu maabara, lugha na KKK;

    e) uratibu wa shughuli za Taasisi na Wakala; na

    f) usimamizi wa utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali.

53. **Mheshimiwa Spika,** katika eneo la *utungaji na utekelezaji wa Sera za Elimu* wizara yangu itatekeleza yafuatayo:

    a) kuanza utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kulingana na Mkakati wa Utekelezaji;

    b) kupitia na kurekebisha sheria na miongozo mabalimbali za elimu ili

kuendana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014;

c) kukamilisha uundwaji wa Mamlaka ya Ithibati na Uthibiti wa Elimu msingi na Sekondari ili kuhakikisha kuwa utoaji wa elimu unazingatia sera, miongozo na mitaala ya elimu yenye kukidhi mahitaji ya soko na jamii;

d) kuimarisha Taasisi ya Elimu Tanzania katika kushughulikia ithibati na uthibiti wa vitabu, zana na vifaa mbalimbali vya elimu msingi na sekondari;

e) kuhuisha mitaala na kuimarisha mfumo wa utoaji wa elimu ya Juu, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kutoa elimu kulingana na mahitaji halisi ya soko la ajira na maendeleo ya Taifa;

f) kuoanisha programu za Elimu ya Juu pamoja na Ufundi ili utoaji wa elimu hiyo uzingatie mahitaji ya soko la ajira ndani na nje ya nchi kwa maendeleo ya Taifa;

g) kuandaa mfumo, miundo na taratibu nyumbufu za kumuwezesha Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali katika mikondo ya kitaaluma na kitaalamu;

h) kuandaa mfumo, muundo mpya wa Taifa wa Tuzo na Tathmini pamoja na kuhuisha taratibu za kujiunga na ngazi

mbalimbali za elimu ili kuendana na muundo mpya wa Taifa wa Tuzo na Tathmini;

i) kuandaa mwongozo wa miundombinu na vifaa vya maabara na mwongozo wa kusimamia utekelezaji wa mitaala kwa kupima na kutathmini maendeleo ya wanafunzi wenye mahitaji maalum;

j) kuandaa mwongozo wa matumizi ya Kiswahili, Kiingereza na Lugha nyingine za kigeni katika kujifunza na kufundishia;

k) kuandaa mikakati ya kutekeleza makubaliano, mikataba, maamuzi ya kikanda na kimataifa ikiwemo kupima kiwango cha utekelezaji wa mpango wa Afrika wa Elimu, malengo ya milenia na maendeleo yanayoishia 2015, na

l) kuendelea kuoanisha mifumo na mitaala ya ngazi zote za elimu na ile ya kikanda na Kimataifa.

54. **Mheshimiwa Spika,** katika eneo la *Ithibati ya Shule,* wizara yangu itatekeleza yafuatayo:

a) itasajili shule za msingi na sekondari kwa kutilia mkazo zaidi shule za ufundi na sayansi pamoja na vituo vya Elimu ya

Watu Wazima na Vituo vinavyotoa Elimu ya Sekondari nje ya Mfumo Rasmi;

b) itaimarisha mfumo na taratibu za usajili wa shule ili kuendana na mahitaji halisi ya soko na maendeleo ya taifa;

c) itaendelea kuelimisha umma kuhusu taratibu za usajili wa shule; na

d) kusajili Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari ili kuthibiti Ubora wa Elimu msingi.

55. **Mheshimiwa Spika,** katika eneo la *Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu* (Uthibiti Ubora wa Elimu msingi) Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:

a) itafuatilia ubora wa elimu katika asasi **17,242**, zikiwemo asasi **8,225** za Elimu ya Msingi na **313** za sekondari zilizokuwa katika utepe mwekundu, asasi **6,672** za Elimu ya Msingi na **1,722** za sekondari zilizokuwa katika utepe wa njano, asasi nyingine 181 za sekondari kwenye mpango wa asasi kwa madaraja wa mwaka 2014/15 na vyuo vya ualimu **129** na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma ili ziinuke katika ubora wa elimu itolewayo;

b) itaimarisha mfumo na taratibu za

Uthibiti Ubora wa Elimu msingi ili kuwa na ufanisi zaidi;

c) itaimarisha ofisi za uthibiti wa ubora wa elimu msingi kwa kuongeza idadi ya wathibiti ubora 570, kutoa mafunzo kwa wathibiti ubora 517, kununua magari 35, kompyuta 782, samani na vifaa vya ofisi kwa ajili ya wilaya mpya zilizoanzishwa; na

d) itakamilisha ujenzi wa ofisi za uthibiti ubora wa elimu msingi za Wilaya za Hai, Urambo, Sumbawanga(M),Masasi, Mtwara (M) na Namtumbo.

56. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia utoaji wa *Mafunzo ya Ualimu* Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:

a) itaendelea kuimarisha ufundishaji wa walimu wa stadi za KKK ikiwemo kuanzisha maabara 7 za lugha katika vyuo vya ualimu chini ya mpango wa LANES/GPE;

b) itaendelea kutekeleza mikakati ya kupunguza uhaba wa walimu wa sayansi na hisabati; na

c) itahuisha Mkakati wa Menejimenti na Maendeleo ya Walimu (TDMS) kwa

kushirikiana na wadau wa maendeleo ya elimu;

57. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia *Taasisi na Wakala,* Wizara itatekeleza yafuatayo:

a) itajenga uwezo wa taasisi za usimamizi wa ubora wa elimu katika ngazi ya elimu ya juu na ufundi na Mafunzo ya Ufundi ili kuhakikisha kuwa elimu bora inatolewa katika ngazi zote za elimu na mafunzo;

b) itainua ubora wa elimu ya juu na ufundi ili kuendana na maendeleo ya kizazi cha tatu na kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 kupitia tafiti na mafunzo yanayokidhi mahitaji ya jamii na stadi za mafunzo;

c) itaimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuweka mifumo ya kidigitali (TEHAMA) itakayowezesha walimu na wanafunzi kupata maandiko muhimu kwa maendeleo ya elimu na Taifa kwa ujumla.

d) itakamilisha miradi ya Afrian Centres of Exellence, Skills for Productive Jobs and Partnership for Applied Science, Engineering and Technology ngazi ya Taifa.

58. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii sasa kueleza malengo ya mwaka 2015/16 ya Taasisi na Wakala zinazosimamia ubora na kuwezesha utoaji wa elimu na mafunzo nchini.

59. **Mheshimiwa Spika,** *Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima* itatekeleza yafuatayo:

    a) itadahili wanafunzi **1,850** katika programu za Astashahada **100,** Stashahada **1,300** na Shahada **450** na kuanzisha programu ya Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii kituo cha Mwanza; na

    b) itapanua wigo wa utoaji wa Elimu changamani baada ya msingi (MECHAM) kutoka Wilaya **13** hadi Wilaya **20** za Tanzania bara.

60. **Mheshimiwa Spika,** *Taasisi ya Elimu Tanzania* imelenga kutekeleza yafuatayo:

    a) itafanya tathmini ya utekelezaji, kupitia (review) na kuboresha mitaala ya Elimu ya Msingi na Ualimu;

    b) itaendelea kutoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa mitaala kwa Walimu,

Wathibiti Ubora wa Elimu, Maafisa Elimu na Waratibu Elimu wa Kata;

c) itaandika vitabu vya kiada kwa shule za msingi na kuhakiki ubora wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia; na

d) itaimarisha miundombinu na kuboresha mazingira wezeshi ya utoaji wa huduma kwa kukarabati jengo la ofisi za Makao Makuu.

61. **Mheshimiwa Spika,** *Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania* itatekeleza yafuatayo:

a) itaimarisha na kuinua ubora wa huduma za Maktaba katika mikoa **21** kwa kuongeza machapisho **50,000** ya watu wazima na watoto;

b) itaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu wa uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za shule, vyuo, taasisi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya nchini;

c) itaendelea kutoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka kwa walengwa **1,000** wa Astashahada, **700** wa Stashahada na **700** wa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya wafanyakazi wa Maktaba; na

d) itaendeleza ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS) Bagamoyo na kuanza

ujenzi wa Maktaba ya chuo pamoja na kukarabati majengo ya Maktaba za Mbeya, Mtwara, Tanga na Sumbawanga.

62. **Mheshimiwa Spika,** *Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu* utatekeleza yafuatayo:

a) itaendelea kutoa mafunzo ya Uongozi wa Elimu kwa viongozi **1,100** wa idara mbalimbali za elimu za Serikali na zisizo za Serikali ngazi ya Shahada **200** na Stashahada **900**. Aidha, mafunzo ya Astashahada kwa Walimu Wakuu wa Shule za msingi **720** kutoka katika mikoa ya Njombe, Mbeya na Iringa yatatolewa chini ya ufadhili wa shirika la Kimataifa la Umoja wa Mataifa la UNICEF;

b) utaendelea kutoa mafunzo ya Stashahada ya Ukaguzi wa Shule kwa wathibiti ubora **240** kutoka katika wilaya zote za Tanzania Bara;

c) utatoa mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi, Uendeshaji na Usimamizi wa Elimu kwa wajumbe **5,000** wa Kamati za shule, **4,000** wa Bodi za Shule, Wakuu wa Shule **300** wa shule zisizo za serikali, Wakaguzi wa Shule **120**, Maafisa Elimu **264** wa Mikoa na

Halmashauri;

d) utatoa mafunzo ya awali (Orientation Course) ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakuu wapya wa Shule za Sekondari **1,500** na Maafisa Elimu wapya **120** wa ngazi ya Halmashauri; na

e) utaongeza fursa za mafunzo kwa kununua eneo la ukubwa wa ekari 100 katika Jiji la Mwanza, kukarabati jengo la zamani la ADEM (Fathers' House) na kuanzisha mafunzo katika kituo cha ADEM tawi la Mbeya.

63. **Mheshimiwa Spika,** *Tume ya Taifa ya UNESCO* itatekeleza yafuatayo:

a) itawezesha wadau kushiriki kupanga na kutekeleza programu za UNESCO katika Nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi ya Jamii, Utamaduni, Habari na Mawasiliano; na

b) itachapisha na kusambaza nakala **700** za toleo la 12 la jarida la Tanzania na UNESCO.

64. **Mheshimiwa Spika,** *Baraza la Mitihani la Tanzania* litatekeleza yafuatayo:

a) litaendesha mitihani ya elimu ya Msingi

kwa watahiniwa **1,200,000** wa Darasa la Nne na **1,045,000** wa Darasa la Saba mwaka 2015;

b) litaendesha mitihani ya elimu ya Sekondari kwa watahiniwa **15,412** wa Maarifa (Qualifying Test - QT), **449,079** wa Kidato cha Pili na **312,363** wa Kidato cha Nne mwaka 2015 na **38,448** wa Kidato cha Sita kwa mwaka 2016; na

c) litaendesha Mitihani ya Ualimu kwa Watahiniwa **22**,**000** mwaka 2016.

65. **Mheshimiwa Spika**, *Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi* litatekeleza yafuatayo:

a) litakagua vyuo **60** kwa ajili ya usajili, vyuo **50** kwa ajili ya kutoa ithibati na kusajili Wakufunzi **400** ili kuthibiti ubora wa elimu;

b) litaratibu udahili wa wanafunzi **60,000** katika ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada katika vyuo vilivyosajiliwa na Baraza;

c) litajenga uwezo wa kutengeneza mfumo wa kuhakiki ubora wa mafunzo katika vyuo vya ufundi **50** pamoja na kufuatilia na kutathimini ubora wa utoaji wa mafunzo katika vyuo **50**;

d) litaandaa mitaala ya kitaifa **15** na kuidhinisha mitaala **50** ya vyuo ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada; na

e) litafanya tafiti **5** na kuratibu mafunzo ya kutumia mitaala inayozingatia umahiri kwa walimu **300**.

66. **Mheshimiwa Spika,** *Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi* itatekeleza yafuatayo:

a) itakamilisha maandalizi na kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe na Rukwa na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha mkoa wa Kagera. Aidha, itaendeleza ujenzi wa chuo cha wilaya ya Namtumbo, kukamilisha maandalizi na kuanza ujenzi wa vyuo vya wilaya za Ukerewe, Chunya na Kilindi pamoja na ukarabati wa vyuo vya Wilaya za Karagwe na Korogwe;

b) itakamilisha ukarabati wa miundo mbinu, ununuzi wa mitambo na zana za kisasa za kufundishia na kujifunzia, kutoa mafunzo kwa Walimu husika *(modernization)* katika Karakana kumi

(10) za Vyuo vya Ufundi Stadi vya mikoa ya Tanga, Mwanza, Moshi na Kihonda Morogoro pamoja na Chuo cha Mafunzo ya Walimu wa Ufundi Stadi cha Walimu cha Morogoro;

c) itaanza ukarabati wa miundombinu, ununuzi wa mitambo na zana za kisasa za kufundishia na kujifunza kwa Walimu husika *(modernization)* awamu ya pili kwa Karakana za Vyuo vya Ufundi Stadi vya mikoa ya Dar es Salaam *Mechatronic*, Dodoma - Ujenzi wa Barabara, Mbeya - Useremala, Iringa - Ufundi wa Magari, Arusha Oljoro – Ufundi wa Zana za Kilimo na Dakawa - Utengenezaji Viatu;

d) itakarabati karakana za Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro *(Morogoro Vocational Teachers Training College - MVTTC)* na kukamilisha ujenzi wa mfumo wa ufundishaji wa masafa;

e) itaendesha mafunzo kwa watumishi wanaofanya kazi katika Sekta Rasmi (makampuni **50**) na mafunzo ya washiriki **3000** walio katika Sekta Isiyo rasmi;

f) itaendesha mafunzo kwa Wanagenzi *(Apprentices)* **500** katika mfumo wa

utambuzi wa ujuzi katika sekta isiyo rasmi *(Recognition of Prior Learning)*;

g) itaanza ujenzi wa mifumo ya TEHAMA *(Local Area Network)* kwa Vyuo vya ufundi stadi vya Singida, Dakawa, Oljoro, Mpanda na Ulyankhulu; na

h) itawajengea uwezo Walimu wa ufundi stadi katika ngazi ya Cheti na stashahada. (Walimu **100** kutoka Vyuo vya VETA na **50** kutoka Vyuo visivyo vya VETA).

67. **Mheshimiwa Spika,** *Mamlaka ya Elimu Tanzania* itatekeleza yafuatayo:

a) itaendelea kutafuta rasilimali fedha kutoka vyanzo mbali mbali ili kufadhili miradi ya Elimu katika ngazi zote kulingana na vipaumbele vya ufadhili; na

b) itaendelea kutekeleza Mpango wa Mamlaka wa Kusaidia Elimu Msingi 2013/2014 – 2015/2016).

68. **Mheshimiwa Spika,** *Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania* itatekeleza yafuatayo:

a) itakagua na kutathmini mipango ya kuanzisha / kuhuisha Vyuo Vikuu 20 na kutathimini program 30 za masomo

toka Vyuo Vikuu nchini ili kusimamia ubora wa elimu itolewayo;

b) itaendelea kuratibu na kusimamia udahili na ukaguzi wa wanafunzi **60,000** ili kufikia lengo la kuwa na wanafunzi **300,000** kwenye Taasisi za Elimu ya Juu nchini ifikapo mwaka 2016;

c) itaanzisha kitengo cha utafiti kitakachoratibu tafiti na kuchapisha makala mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya elimu ya jamii;

d) itaratibu upatikanaji wa wanataaluma **30** toka Vyuo Vikuu Nchini watakaojiunga na Masomo ya Uzamili na Uzamivu chini ya makubaliano ya Serikali ya Tanzania na Ujerumani (DAAD); na

e) itaanza ujenzi wa ofisi za kudumu za Tume katika kiwanja cha Uporoto, Dar es Salaam.

69. **Mheshimiwa Spika,** *Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu* itatekeleza yafuatayo:

a) itakusanya shilingi **51,001,034,808.24** za marejesho ya mikopo iliyotolewa kati ya mwaka 1994/95 na 2014/15;

b) itatoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji **101,129** wakiwemo wa stashahada ya Ualimu na 'DAAD' kati yao **23,297** wa mwaka wa kwanza na **77,832** wanaoendelea na masomo pamoja na kutoa ruzuku kwa wanafunzi **1,963** wanaosomea mafunzo ya shahada ya afya za binadamu na wanyama; na

c) itaanza kutekeleza mpango wa kutumia Mfumo wa kielektroniki (Enterprise Resource Planning (ERP) Solution) katika shughuli za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;

70. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii sasa kueleza malengo ya mwaka 2015/16 ya Taasisi na Wakala zinazotoa elimu na mafunzo. Wizara yangu ina jumla ya Taasisi **51** zinazotoa mafunzo nje ya mfumo wa mafunzo ya ufundi stadi. Taasisi hizi ni pamoja na Vyuo vikuu **12**, Vyuo vya Ufundi **5** na Vyuo vya Ualimu **34**. Taasisi hizi zina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo husika. Katika mwaka 2015/16, zitatekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:

71. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo cha*

*Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi **4,000** katika programu mbalimbali kati yao **1,000** wa Astashahada, **1,500** Stashahada na **1,500** shahada ya kwanza pamoja na kuanzisha mitaala mipya **10** ngazi ya cheti na diploma na kuanzisha programu **4** za uzamili katika fani za sayansi ya jamii, elimu, tehama na elimu;

b) kitaajiri wanataaluma **57** kati yao **18** wa uzamivu, **23** uzamili na **16** shahada ya kwanza pamoja na wafanyakazi waendeshaji **28** pamoja na kugharimia mafunzo ya watumishi **2** katika ngazi ya shahada ya uzamili na **6** katika ngazi ya shahada ya uzamivu na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi waendeshaji **8** na wahadhiri **8**;

c) kitaendeleza ujenzi wa hosteli ya wanafunzi katika Kampasi ya Kivukoni pamoja na kukarabati nyumba **3** za wafanyakazi; na

d) kitafanya tafiti mbalimbali za maendeleo katika nyanja mbalimbali

ikiwemo uongozi, jinsia, mazingira, uchumi, maendeleo ya jamii, elimu na nyinginezo.

72. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo cha Ufundi Arusha* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi **690** wa mwaka wa kwanza (Astashahada **40** na Stashahada **600**, Shahada **50**);

b) kitahuisha mitaala 12 ya programu zilizopo za Ufundi Sanifu (NTA 4-6) na kuanzisha programu ya Ufundi Sanifu (NTA 4-6) katika fani za Magari na Mitambo mikubwa na Stashahada ya Mafunzo ya Ualimu wa Sayansi;

c) kitaajiri wafanyakazi **35** kati yao waendeshaji **15** na wanataaluma **20** pamoja na kugharimia mafunzo kwa wafanyakazi **15** kati yao wanataaluma **10** na waendeshaji **5**;

d) kitajenga jengo la ofisi za kitaaluma (Ufundi Block), kufanya ukarabati na kununua vifaa vya Karakana na Maabara (Civil, Electrical, Mechanical and ICT) na samani za Jengo la Uhandisi Umwagiliaji pamoja na kuendeleza

jitihada za kutafuta chanzo cha maji katika shamba la Oljoro; na

e) kitatekeleza Mpango Mkakati wa kuhuisha kituo cha mafunzo ya kutengeneza mashine ndogo za kuzalisha umeme kwa kukarabati kituo cha kuzalisha umeme cha Kikuletwa pamoja na kuendelea kufanya tafiti za Kisayansi na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za Sayansi na Teknolojia.

73. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi wa Shahada ya Kwanza **8,500**, Uzamili **2,500** na Uzamivu **500,** kuanzisha Shule Kuu ya Usanifu wa Majengo na Mipango Miji pamoja na kuendeleza ujenzi wa Mradi wa Buyu;

b) kitakarabati miundombinu ya kufundishia, umeme, maji taka, makazi ya wanafunzi, njia za kupita na mazingira ya kufanyia utafiti, kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa ya nyongeza kwa ajili ya Shule Kuu ya Sayansi za Afya na kuanza maandalizi ya ujenzi wa kituo cha wanafunzi

(Student Centre);

c) kitaajiri wafanyakazi wapya **300** ili kukidhi mahitaji ya programu mpya zilizoanzishwa na kujaza nafasi zilizoachwa wazi pamoja na kugharimia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi;

d) kitaimarisha mfumo wa kudhibiti ubora wa elimu na mafunzo na kusimamia utekelezaji wake (Quality Assurance and Control); na

e) kitakamilisha mipango ya utekelezaji wa ujenzi wa ofisi, hoteli na hosteli kwa njia ya ubia na sekta binafsi (PPP).

74. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi **1,800** (**500** wa fani ya Sayansi, **150** hisabati, **280** lugha) wa Shahada ya Kwanza na kupata ardhi nyingine kubwa zaidi kwa ajili ya upanuzi wa chuo;

b) kitaajiri jumla ya wafanyakazi **50** kati yao walimu **40** na waendeshaji **10**, kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wenye

mahitaji maalumu pamoja na vifaa vya maabara, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na kukarabati miundombinu ya umeme;

c) kitakarabati barabara, majengo ya Kitivo cha Sayansi za Jamii na Humanitia, Utawala, Maabara na Madarasa katika shule ya Sekondari ya Mazoezi, kujenga uzio wa chuo (fence Phase II) na kuzuia mmomonyoko wa udongo katika hosteli ya Mbagala; na

d) kitaendelea kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hususan kwa shahada za uzamili na uzamivu.

75. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka **1,284** mwaka 2014/15 hadi **1,500** mwaka 2015/16 (**960** wa fani ya Elimu ya Jamii na Ualimu, **300** Sayansi ya Ualimu, **120** Elimu katika Sayansi, na **120** Elimu katika Elimu ya Jamii), na kuanzisha program mpya **2** za shahada ya kwanza, **2** uzamili na **3** za masomo yasiyokuwa ya shahada;

b) kitakamilisha ujenzi wa ukumbi wa

mihadhara, kukarabati madarasa, kumbi **2** za mihadhara, maktaba, maabara **2**, mabweni **6**, ofisi za wafanyakazi, miundombinu ya maji, barabara, umeme na mawasiliano;

c) kitaajiri wafanyakazi wapya **142** kati yao wanataaluma **95** na waendeshaji **47** pamoja na kugharimia masomo ya wahadhiri **20** kati yao wa shahada ya uzamili 4 na uzamivu 16; na

d) kitaimarisha uwezo wa chuo katika kufanya utafiti (basic & applied research) ambao unalenga kutatua matatizo ya jamii.

76. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi **3,749** kati yao wanafunzi wa Shahada ya Kwanza **3,000**, Uzamili **238**, Uzamivu **70**, Stashahada **373** na astashahada **68**;

b) kitaanzisha program nne mpya za Shahada za kwanza za Bachelor of Community Development, BSc. Computing and Information Technology, BSc Computing with Education (IT and Mathematics) na BSc Lather Production

and Processing;

c) kitaanzisha program sita mpya za Shahada za uzamili za MSc. in Agricultural Statistics, MSc in Project Planning, Management and Evaluation, Postgraduate Diploma in Result Based Monitoring and Evaluation Techniques, MSc. Environmental Science, Management and Technology, MSc. Hydrogeology and Water Resources Management na MSc. of Philosophy (Mphil-Veterinary)

d) kitaimarisha vitengo vya uzalishaji kwa kuhakikisha Kampuni ya "SUA Investments Ltd" inaanza kufanya kazi; na

e) kitakamilisha ujenzi wa maabara kwa ajili ya Kitivo cha Sayansi inayogharimiwa na mradi wa EPINAV; na

f) kitakamilisha ujenzi wa upelekaji maji Kampasi ya Solomon Mahlangu na kukarabati maktaba iliyopo Kampasi Kuu, paa la maabara ya Idara ya Sayansi ya udongo na maabara ya Idara ya Sayansi ya Wanyama na Uzalishaji.

77. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi,* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi **2,229** wa mwaka

wa kwanza na kugharimia mafunzo ya wafanyakazi **50** katika ngazi za Uzamili **21** na Uzamivu **29**;

b) kitakarabati Maktaba, Hosteli, Kumbi za Mihadhara katika Kampasi ya Moshi pamoja na Jengo la ofisi na Mabweni katika Kampasi ya Kizumbi;

c) kitafanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalam na kuchapa makala mbalimbali kwa kushirikiana na vyuo vingine vya ndani na nje ya nchi kwa lengo kusambaza elimu inayokidhi mahitaji ya sasa ya jamii ili kupunguza umaskini;

d) kitakarabati ofisi za Mikoa ya Mtwara, Iringa, Mwanza na Singida; na

e) kitaendelea kutoa elimu ya ushirika nje ya Chuo ili kuchochea ari ya maendeleo katika jamii kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwemo Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) na Shirikisho wa Vyama vya Ushirika (TFC).

78. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu Huria cha Tanzania* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi **12,000** wakiwemo

Astashahada **4,000**, Shahada ya Kwanza **3,500**, Uzamili **4,500;**

b) kitatekeleza mpango wa utoaji wa mitihani kadri ya maombi ya wanafunzi (On Demand Examination - ODEX);

c) kitajenga jengo la maabara ya Sayansi na jengo la madarasa na mihadhara Makao Makuu Bungo - Kibaha, majengo ya vituo vya mikoa ya Manyara na Mwanza pamoja na kukarabati majengo ya mikoa ya Lindi, Rukwa, Kinondoni na Dodoma;

d) kitaimarisha matumizi ya TEHAMA, kuweka vitini (study materials) na vitabu vya masomo kwenye mifumo ya digitali na kuanzisha Maktaba ndogo katika vituo vya mikoa / uratibu ili wanafunzi waweze kujifunza kwa urahisi; na

e) kitafanya tafiti katika maeneo ya Mazingira, Nishati, Kilimo na Chakula, Elimu, TEHAMA, Uongozi na Biashara, Maendeleo ya Utalii, Sheria, Udhibiti wa Ubora, Utawala na Maendeleo, Watu Wenye Ulemavu na Mahitaji Maalum, Maliasili, Umaskini, Utamaduni, Haki za Binadamu, Maendeleo ya Watu na Mawasiliano pamoja na kuongeza idadi na upatikanaji wa Jarida za tafiti na

majarida ya ki-elektroniki (e-journals and periodicals**)** katika vituo vya mikoa / uratibu.

79. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu cha Ardhi* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi **4,087** wakiwemo wa Shahada ya Kwanza **3,872**, Stashahada ya Uzamili **10**, Uzamili **180** na Uzamivu **25** na kununua eneo kwa ajili ya upanuzi wa ujenzi wa Chuo;

b) kitakamilisha ujenzi wa "Lands Building", kuanza ujenzi wa hosteli, jengo la studio kwa ajili ya wanafunzi wa shahada ya Usanifu Majengo, kituo cha wanafunzi, nyumba ya Makamu Mkuu wa Chuo, upanuzi wa maktaba na kuendeleza miundombinu ya TEHAMA;

c) kitafanya tafiti **51** katika maeneo yahusuyo matumizi bora ya rasilimali ardhi, ujenzi na usanifu majengo, usimamizi wa mazingira na maeneo mengine na kutoa machapisho **28**; na

d) kitatoa huduma za ushauri elekezi katika fani ya maendeleo ya ardhi, ujenzi na usimamizi wa mazingira katika miradi nane **(8)** na kutoa huduma kwa jamii kupitia "Public Outreach Programs" sita **(6)**.

80. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi **1404** wakiwemo Stashahada **340**, Shahada ya Kwanza **660**, Uzamili **340** na Uzamivu **4**;

b) kitafanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusiana na afya za binadamu ikiwemo; majaribio ya chanjo dhidi ya maambukizi ya VVU kwa ushirikiano na wadau wa ndani nan je ya nchi; uchunguzi wa magonjwa ya Kifua Kikuu na Malaria na ugonjwa wa kurithi wa chembechembe nyekundu za damu (Sickel Cell);

c) kitaendelea na ujenzi wa Hospitali ya kufundishia ya Mloganzila na kutoa huduma pamoja na kuweka vifaa Tiba na kuanza ujenzi wa mabweni ya wanafunzi, hosteli za interns, na nyumba za wafanyakazi;

d) kitaajiri watumishi **968** katika Hospitali ya kufundishia na kutoa huduma baada ya ujenzi wa Hospitali kukamilika mwezi Juni 2016; na

e) kitakarabati hosteli, Majengo ya Utawala, Maabara, Maktaba, Tiba za asili na nyumba za wafanyakazi.

81. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu Mzumbe* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi **4,195** wakiwemo Astashahada **250**, Stashahada **370**, Shahada ya Kwanza **2,120**, Uzamili **1,450** na Uzamivu **5**;

b) kitajenga madarasa **5**, kampasi kuu, kujenga madarasa na ofisi kampasi ya Mbeya, kukarabati mabweni manne (**4**) ya wanafunzi kampasi kuu na kujenga Kituo cha Wanafunzi (Student Services Centre), na kukarabati jengo la mafunzo ya juu na utafiti katika Kampasi Kuu Mzumbe;

c) kitagharimia mafunzo watumishi **27** (Uzamili **17** na Uzamivu **10**) ili kuimarisha ubora wa mafunzo yatolewayo;

d) kitachapisha vitabu **8**, makala za kufundishia **2** na makala nyingine **36** pamoja na kukamilisha tafiti katika maeneo **20** na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo **25** ya Menejimenti, Uongozi na Sayansi ya Jamii; na

e) kitafanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam.

82. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu cha Dodoma* kitatekeleza yafuatayo:

a) kitaongeza fursa za kujiunga na Elimu kwa kudahili wanafunzi **11,782** wakiwemo Stashahada **3,526**, Shahada ya Kwanza **7,663** na Uzamili **593**;

b) kitaendeleza ujenzi wa Vyuo vya Tiba, Sayansi Asilia, Hisabati, Sayansi za Ardhi na miundombinu ya maji safi na taka pamoja na kuanza ujenzi wa nyumba za wafanyakazi pamoja na kununua samani za madarasa, ofisi, mabweni, maabara na nyumba pamoja na magari 20, kompyuta, vifaa vya kufundishia vikiwemo vya maabara; na

c) kitaendeleza utafiti katika maeneo ya mazingira, rasilimali, uchumi na tabia nchi.

83. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mwalimu Julius K. Nyerere Butiama* kimeanzishwa kwa lengo la kuongeza idadi ya wataalamu katika fani za Sayansi, Teknolojia na Kilimo. Katika mwaka 2015/16 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

a) kitadahili wanafunzi **800** (Stashahada **40** na Shahada **760)** kwa kutumia majengo ya Oswald Mang'ombe;

b) kitaajiri watumishi wakiwemo wanataaluma **80** na waendeshaji **20**; na

c) kitaanza ujenzi wa jengo la Shule Kuu ya Kilimo.

84. **Mheshimiwa Spika,** katika Usimamizi na Utekelezaji wa Programu na Miradi, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:

**a) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu**

kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya mwalimu (Teacher Development management Strategy); na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu za Elimu.

**b) Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa**

i. kupanga madaraja ya shule kulingana na ufaulu (Official School Ranking);

ii. kutoa mafunzo ya Kujenga Uwezo wa Walimu na Wanafunzi kwa shule za Msingi (STEP primary);

iii. kutoa mafunzo ya Kujenga Uwezo wa Walimu na Wanafunzi kwa shule za Sekondari (STEP Secondary);

iv. kuwezesha utoaji wa motisha kwa shule na Halmashauri zilizoonyesha mafanikio katika matokeo ya mitihani ya kidato cha nne na darasa la saba;

v. kuwezesha ujenzi wa nyumba **40** za Walimu katika maeneo yasiyofikiwa kwa urahisi; na

vi. kuwezesha uratibu, ufuatiliaji na uendeshaji wa shughuli za Miradi ya Elimu, ikiwemo miradi ya BRN

**c) Kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu**

i. kukamilisha maandalizi na kuanza ukarabati wa vyuo 6 vya ualimu, ujenzi wa vyuo vya mikoa vinne (4) vya Ufundi stadi na ujenzi wa hosteli Morogoro VTTC , jengo la maabara katika Chuo cha Ufundi

Arusha;

ii. kununua mitambo, zana na vifaa vya kufundishia, vitabu, vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya Chuo cha Ufundi Arusha, vyuo vya ualimu na Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro;

iii. kujenga uwezo wa vyuo vya ualimu nchini katika kuandaa walimu wa sekondari katika fani za sayansi nateknolojia; na

iv. kujenga uwezo wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi katika kuandaa na kufundisha mitaala inayozingatia umahiri.

**d) Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi**

i. kuandaa zana za kufanyia tathmini endelevu ya upimaji stadi za KKK na kuingiza katika mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za ubora wa shule, kukamilisha kiunzi cha udhibiti wa ubora pamoja na kujenga uwezo wa matumizi ya kiunzi hicho;

ii. Kukamilisha Mwongozo wa

Mwalimu wa Stadi za Maisha na kuchapisha vitabu vya stadi za maisha kwa madarasa ya 1&2, 3&4 na 5-7;

iii. kuendesha mafunzo kuhusu KKK kwa Maafisa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Walimu wa Darasa la I, II, III na IV, Wakufunzi wa Uwezeshaji, Walimu na Wanafunzi kuhusu TEHAMA, Maafisa 100 kuhusu Utafiti wa KKK, na Uwekaji wa Mikakati ya Mazingira rafiki shuleni; na

iv. kujenga uwezo wa watendaji katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri juu ya matumizi sahihi ya mwongozo wa Huduma ya Maji, Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni.

**e) Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari**

i. kufuatilia ujenzi na upanuzi wa miundombinu katika shule **528** na tathmini ya matokeo (Impact Assessment) ya shule **264** katika halmashauri **132**;

ii. kuimarisha Hazina Data na Mfumo wakukusanya, kuchakata na kuhifadhi takwimu, kufanya mapitio ya zana za kukusanya

takwimu pamoja na kuwezesha utoaji mafunzo kwa watumishi wa kitengo cha takwimu;

iii. kutoa mafunzo kazini kwa walimu **10,000** wa shule za sekondari nchini;

iv. kuzijengea uwezo taasisi za ithibati ya Elimu Msingi, ADEM, TIE na NECTA; na

v. kufanya ufuatiliaji wa ruzuku za uendeshaji wa shule katika Halmashauri na ukaguzi wa mahesabu ya Mradi

**f) Mradi wa Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA**

i. kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

**g) Mradi wa Kuimarisha Mfumo Mpango wa Elimu kwa Waliokosa (YES I CAN)**

i. kuwajengea uwezo wawezeshaji **100** wa vituo vipya **20** vilivyoko katika Halmashauri zenye watu wengi wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu; na

ii. kuwezesha uratibu, ufuatiliaji

na tathmini ya vituo vya kisomo cha NDIYO NINAWEZA katika Halmashauri **20**.

h) **Mpango wa Kuongeza Ujuzi wa Kuweza Kuajiriwa au Kujiajiri (Improving Skills Training for Employment Program-ISTEP 2014-2019)**

i. kuanza kutoa mafunzo katika Sekta za Utalii, Gesi Asilia, Mafuta na Madini kwenye vyuo **6** vya Tanzania vya awamu ya kwanza kwa kushirikiana na vyuo **6** vya Kanada ambavyo tayari wameshaingia navyo ubia; na

ii. kufanya mchakato wa vyuo **5** vya Tanzania ili viingie ubia na vyuo **5** vya Kanada katika Sekta za Utalii, Gesi Asilia, Mafuta na Madini na kuanza kutoa mafunzo Januari, 2015.

85. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake kulingana na vipaumbele vya mwaka 2015/16, wizara inatarajia kutumia jumla ya **Shilingi 989,552,542,000.00.** Kati ya fedha hizo shilingi **510,877,383,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **478,675,159,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

## VI. SHUKRANI NA HITIMISHO

86. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kuongoza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kipindi cha miaka mitano tangu mwaka 2010 hadi mwaka 2015. Aidha, nachukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta (Mb.), waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wazazi, Wahadhiri, Wakufunzi, Walimu, Wanafunzi na Watanzania wote kwa ujumla kwa ushirikiano wenu mlionipa katika kipindi chote cha uongozi wangu. Shukurani za pekee ziende kwa wananchi wangu wa Jimbo la Bagamoyo kwa kuendelea kuniamini na kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa kipindi hiki cha miaka 5.

87. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwashukuru wadau wote wa sekta ya elimu, wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Asasi za Kiraia, viongozi mbalimbali na wananchi ambao wamechangia katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya Elimu na Mafunzo.

88. **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya Washirika

wa Maendeleo ambao wamechangia kufanikisha mipango ya Elimu na Mafunzo ni pamoja na serikali za: Algeria, Australia, Canada, China, Cuba, Denmark, India, Japan, Marekani, Misri, Msumbiji, Norway, Finland, Netherlands, Pakistan, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi na Uturuki. Aidha, mashirika yaliyochangia katika kufanikisha programu za Elimu na Mafunzo ni pamoja na: Aga Khan Education Services, Airtel, Barclays Bank, Benki Kuu, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Taifa ya Biashara, Book Aid International, British Council, CAMFED, Care International, Children International, Children's Book Project, DFATD, COL, Commonwealth Secretariat, CRDB, DAAD, DANIDA, DfID, EDC, FEMINA, Ford Foundation, GIZ, ILO, International Reading Association, Irish Aid, JICA, JOVC, KOICA, Mwananchi Communications, NMB, NORAD, NUFFIC, OPEC, Oxfam, Peace Corps, Plan International, Rockefeller, Shirika la Volkswagen, Sida, Sight Savers International, TENMET, Tigo, Umoja wa Nchi za Ulaya (European Union EU), UNAIDS, UNDP, UNESCO, UNESCO Institute for

Life Long Learning (UIL), UNFPA, UNICEF, USAID, VODAC, VSO. KUHN International GmbHg, CICan Taasisi mbalimbali duaniani vinavyoshirikiana nasi.

## VII. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/16

89. **Mheshimiwa Spika**, kwa taarifa hii, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2015/16 ya jumla ya Shilingi **989,552,542,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:

a) Shilingi **109,022,940,370.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara na Vitengo ambapo Shilingi **70,993,671,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **38,029,269,370.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

b) Shilingi **401,854,442,630.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Taasisi. Kati ya hizo, Shilingi **325,024,671,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara, na Shilingi **76,829,771,630.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

c) Shilingi **478,675,159,000.00**

zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi **446,578,000,000.00** ni Fedha za Ndani ambapo Shilingi **348,300,000,000.00** ni kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu sawa na asilimia **78** ya Fedha za Ndani na Shilingi **32,097,159,000.00** ni Fedha za Nje (Washirika wa Maendeleo).

90. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wizara yangu, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

91. **Mheshimiwa Spika**, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya: http://www.moe.go.tz.

92. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.